**MAJALIWA** awapa jukumu ma-DAS kukabili ushoga

UKURASA 19



**MAJAJI** wamvaa Rostam tuhuma dhidi ya korti

UKURASA 19


Wafuatiliaji watafuta sababu wazungumzaji Kiswahili kuongezeka kufikia milioni 500

Waambiwa tafuteni mbinu za kuingia ulingoni kutoka kwa watangulizi wenu

siasa

JUMATANO JULAI 5, 2023 Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

DK. OMAR ALLY JUMA Makamu wa Rais wa kwanza, ndani ya vyama vingi, juhudi, kazi alizoasisi bado zinang'ara

Wadau wanavyoshangilia kuengua wakurugenzi kusimamia uchaguzi

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Julai 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581362

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Waziri azionya taasisi za dini

**AMTAJA** Zumaridi ukiukwaji wa maadili...

*Endelea ukurasa wa 2*


Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni

Mfalme Zumaridi

MAZUNGUMZO MAALUM



# Lissu asema nia urais iko palepale

**MBADALA** wake atawania ubunge; achambua kikokotoo cha mafao...

*Endelea Uk. 3*




Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa mikataba mitatu ya msaada uliotolewa na Umoja wa Ulaya (EU), kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El-maamry Mwamba (kulia) na Balozi wa EU nchini, Manfredo Fanti, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia aahidi usimamizi mkali wa matumizi Trilioni 1.7/- zilizotolewa na EU

UKURASA 2

**MICHEZO** **ROBETINHO ANOGESHA USAJILI SIMBA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa heshima za mwisho kwenye mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Francis Mtega, katika viwanja vya polisi Chimala wilayani Mbarali mkoani Mbeya jana. **Habari Uk. 3.** **PICHA: OWM**

# Waziri aonya taasisi za dini

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesema kuna baadhi ya taasisi za dini zinajiendesha kinyume cha tamaduni za kitanzania na kuzionya kuwa zitachukuliwa hatua, ikiwamo inayoendeshwa na Diana Bundala, maarufu Mfalme Zumaridi, anayejiita Mungu.

Masauni amesema miongoni mwa taasisi ambazo zinakwenda kinyume ni zile ambazo hazijasajiliwa, likiwamo Kanisa la Zumaridi.

Waziri huyo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua kikao kati yake na viongozi wa mashirikisho na mabaraza ya kidini.

Alisema taasisi inaposajiliwa inapata udhamini kutoka kwa mdhamini wao, hivyo ni muhimu kujiridhisha wanapowachukulia dhamana ili wafuate yale yanayotakiwa.

"Zipo taasisi ambazo zinaibuka kama huyo Zumaridi. Hajasajiliwa! Ametoka huko anajiita yeye ni kiongozi wa dini. Utakuta wengine wanahamasisha mapenzi ya jinsia moja, mwingine anajiita yeye ni Mungu, wanazungumza mambo ya ajabu ambayo hayawezi kukubalika," alionya Masauni.

Waziri huyo alisema serikali haiwezi kukubali na wamekuwa wakichukua hatua kwa wale wote wanaokwenda kinyume cha sheria ya nchi, kimaadili, mila na desturi za nchi.

"Jeshi la Polisi lipo, mtu akiiba anakamatwa na taasisi za dini na viongozi wa dini au unatumia dini... mtu yeyote atachukuliwa hatua, simzungumzii huyo mtu mmoja na wengine wanaokiuka taratibu, hatua zitachukuliwa kwa yeyote anayevunja sheria za nchi," alisisitiza.

Masauni alisema changamoto iliyopo kwa sasa ni kuanzishwa kwa taasisi za kidini pasipo kufuata sheria. Hatua zitachukuliwa.

"Zipo taasisi nyingi katika jamii yetu ambazo zinajiendesha pasipo kusajiliwa na hata uendeshwaji wake ni wa kutia shaka. Nitoe wito tusaidiane katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kusajili jumuiya na vikundi," alisema Masauni.

Aliwaeleza viongozi hao kwamba inapobainika kuna jumuiya au vikundi vya kidini ambavyo uendeshwaji wake unatia shaka, ni vyema wakatoa taarifa Ofisi ya Msajili katika kuzibaini ili kuweka jamii katika hali ya usalama na amani.

"Hivi karibuni nchi yetu imeekumbwa na viashiria vya uvunjifu wa maadili ya kijamii. Kwa niaba ya wizara, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi ambao mlijitokeza na kukemea kwa uwazi vitendo ambavyo si utamaduni wetu na vinatweza utu wetu," alisifu Masauni.

Waziri huyo alisema vita dhidi ya uvunjifu wa maadili ni ya watu wote. Vitendo visivyo na maadili vipingwe pasipo kuoneana.

Masauni alisema serikali na taasisi za kidini kila upande ukitimiza wajibu wake anaamini jamii itakuwa salama.

"Nichukue fursa hii kuwasihi viongozi wetu wa kiroho, kutoleta taharuki katika jamii kutokana na mafundisho mnayoyatoa yanaweza kutugawa katika kupambana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili.

"Sitaki kuonekana kama mwalimu au mtafsiri wa sheria, lakini sisi sote tunatambua kuwa serikali yetu haina dini isipokuwa watu wake wana dini na wanaamini katika imani tofauti tofauti.

"Katiba yetu inatoa haki kwa Watanzania kuamini katika imani waitakayo bila kuingiliwa mradi tu katika kutekeleza haki hiyo hawavunji sheria," alifafanua.

Waziri huyo alisema ili kuweka utaratibu mzuri kwa taasisi za kidini katika kujiendesha, Bunge limetunga sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Jumuiya Sura ya 337.

"Sheria hii inahusika na kusajili na kusimamia jumuiya zote kwa ujumla wake ikiwamo na taasisi za kidini," alikumbusha.

Masauni alisema ni wajibu wa viongozi wa dini kuhakikisha jumuiya wanazoziongoza zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria kwa kutekeleza masharti ya usajili wa jumuiya ambayo ni kuwasilisha taarifa mbalimbali kila mwaka kama ilivyoelekezwa katika sheria na kulipa ada kwa wakati.

Masauni aliwataka kuzingatia masharti ya usajili na sheria zingine za nchi katika kuendesha shughuli za jumuiya wanazoziongoza.

Alisema hivi karibuni kumekuwa na migogoro mingi inayozikumba jumuiya za kidini na kutumia muda na rasilimali nyingi katika kushughulika na utatuzi wa migogoro badala ya rasilimali hizo na muda kutumika kutoa huduma kwa waumini wao.

Alisema uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya umebaini migogoro mingi inatokana na katiba za muda mrefu ambazo kwa mazingira ya sasa zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

"Jambo lingine ni kutokuwa na uwazi katika mapato na matumizi ya taasisi, kugombea madaraka na viongozi na wafuasi au waumini kutokuwa na uelewa wa katiba yao na sheria zinazosimamia uendeshaji wa jumuiya," alisema Masauni.

Alisema katika eneo la migogoro, viongozi wa dini wanatakiwa kufanya mapitio ya katiba zao na kujiridhisha kama zinakidhi haja kwa wakati uliopo.

Masauni pia alisema kuna haja ya kujengeana uwezo wa kuzieleza katiba zao na miongozo iliyopo na kuendesha taasisi kwa kuzingatia katiba kutasaidia kuepusha migogoro isiyokuwa na sababu.

"Pia katika kusimamia rasilimali za taasisi ni vizuri kuwa na uwazi ambao utawasaidia waumini au wanachama kujua jinsi mapato na matumizi ya taasisi yalivyo," alieleza.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania (ACT), Mahimbo Mndolwa, alisema kikao hicho ni fursa kushirikiana na kujadiliana magumu ambayo wanakutana nayo.

Mchungaji wa Kanisa la Maombezi (GRC), Anthony Lusekelo, alisema asilimia 90 ya Watanzania wanasali, hivyo ni lazima kuwapo na uhusiano mzuri na taasisi za dini ili kuwe na manufaa makubwa kwa maslahi ya nchi.

Alisema ni vizuri serikali kwa zile taasisi ambazo zinajiendesha kinyume cha maadili zikafutiwa usajili na kuchukuliwa hatua kali.

"Kama kuna hizo taasisi za dini zinahamasisha mapenzi ya jinsia moja, serikali izikatae kuzitambua kisheria, tuvunje ushirikiano kwa maana ya kuzifutia usajili na hatua za kisheria zichukuliwe, itakapojiridhisha hatua kali zichukuliwe," alishauri.

# Samia aahidi usimamizi mkali matumizi fedha walizotoa EU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali anayoiongoza itasimamia ipasavyo matumizi ya fedha zilizotolewa na Umoja wa Ulaya (EU) Sh. trilioni 1.71 kwa ajili ya bajeti ya serikali ya mwaka 2023/24.

Umoja huo umetoa fedha hizo kwa Tanzania baada ya kuvutiwa na utendaji kazi wa Rais Samia katika kuleta mabadiliko ya sera na utawala wa kijinsia.

Akizungumza jana baada ya kushuhudia utiaji saini mikataba mitatu ya kifedha jijini hapa, Rais Samia alisema fedha hizo zitasaidia katika mapitio ya sera, uchumi wa buluu, jinsia, sekta ya kidigitali, uboreshaji wa barabara vijijini, nishati na kilimo.

"Tunashukuru kwa msaada huu mkubwa, Umoja wa Ulaya ni moja ya wadau wetu muhimu wa maendeleo katika kufikisha huduma muhimu kwa wananchi wetu," alisema.

Rais Samia alisema fedha hizo zitasaidia maendeleo ya Tanzania na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo awamu ya tatu.

Alisema katika majadiliano yake mapema jana na Balozi wa Umoja huo nchini, Manfredo Fanti ambaye anamaliza muda wake, alimwachia mambo matano na kumhakikishia atafanyia kazi.

"Ninaomba uende na maombi yangu matatu; Tanzania inatekeleza programu ya BBT tunategemea kutumia Benki ya Maendeleo ya Tanzania na Benki ya Uwekezaji kuwezesha vijana na wanawake waliopo katika programu hii, hivyo ninaomba EU kukubali kujumuisha benki mbili ambazo ni Benki ya Kilimo na Benki ya Uwekezaji kwa kuwapa mikopo kwa ajili ya programu hii.

"Pia kukamilisha mpango mpya wa kuendeleza ushirikiano kati ya Tanzania na EU kwa kuwa ni shauku kwetu kujua ushirikiano wetu ili tujiandae na makubaliano hayo," alisema.

Rais Samia aliomba kuongeza mradi wa ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza na miundombinu yake itakayowezesha 'hata majirani' kwenda kupata huduma.

Alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kufanya kazi kwa karibu na umoja huo na makubaliano yenye manufaa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mikataba hiyo ni mwendelezo wa mpango mkakati wa miaka saba (2021 hadi 2027) wa kusaidia Serikali ya Tanzania.

Alisema Benki ya Uwekezaji ya Ulaya imekuwa chombo muhimu cha kuiwezesha Tanzania katika miradi ya maendeleo.

"Imewezesha maboresho ya viwanja vya ndege katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Kagera, Rukwa na Shinyanga, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, pia kusaidia mikopo kwa benki za kibiashara ili kusaidia wanawake na vijana," alisema.

Awali Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El-Maamry Mwamba, katika ziara ya Rais Samia aliyoifanya Februari 2022 Ubelgiji na kukutana na Rais wa EU imeleta matunda hayo.

"Mkataba wa kwanza ni utekelezaji wa mradi wa uchumi wa buluu ambao umegharimu Sh. bilioni 279 utakaoleta mabadiliko ya tabia nchini kwenye pwani za Tanzania Bara na Zanzibar. Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha na kukuza sekta binafsi Sh. bilioni 160 zitatumika.

"Mkataba wa tatu ni kuimarisha uhusiano katika nchi za Umoja wa Ulaya katika kuongeza ufanisi katika kubuni miradi inayosimamiwa na EU yenye gharama ya Sh. bilioni 15.23," alisema.

HABARI KITAIFA

# Lissu asema bado ana nia ya urais

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, ameweka hadharani kwamba bado ananuia kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu ujao, chini ya angalizo iwapo katiba mpya itapatikana.

Lissu (55), ameiambia Nipashe wiki hii kwamba iwapo chama chake hakitampitisha kuwania nafasi hiyo, mbadala wake ni ubunge, ingawa hakuwa tayari kutaja jimbo husika.

“Ni uamuzi wa mchakato wa chama, kamati kuu, baraza kuu na mkutano mkuu kama ilivyokuwa 2020 au waliogombea kabla yangu. Chama kitakapotuita nitaitika wito, nitaitika wito wa chama,” Lissu alitamka, huku akirejea mwongozo wake mkuu ni katiba ya chama.

Hata hivyo, Lissu alieleza ishara za hisia kwamba sehemu mojawapo anayoweza kwenda kugombea pale itakapobidi, ni Jimbo la Singida Mashariki, alikokuwa mbunge kabla ya kujeruhiwa na kuondoka nchini.

Katika Uchaguzi Mkuu uliopita, ambao Lissu aligombea urais na kushika nafasi ya pili nyuma ya Dk. John Magufuli wa CCM, CHADEMA ilipata mbunge mmoja, Jimbo la Nkasi Kaskazini, mkoani Rukwa.

**KATIBA MPYA**

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, pia amezungumzia suala la Katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, akisisitiza msimamo wa chama hicho kwa sasa ni kutokushiriki uchaguzi wa aina yoyote ikiwamo uchaguzi wowote mdogo, uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani na hata Uchaguzi Mkuu wa mwaka ikiwa haitopatikana tume huru ya uchaguzi.

“Nchi itaingia kwenye matatizo makubwa, hicho ndicho ninachoweza nikakisema waziwazi kabisa ama tutapata katiba mpya ama tutarudi kwenye utawala wa Magufuli bila Magufuli.

“Kwa hiyo ni ama tutapata katiba mpya tufanye uchaguzi huru na wa haki au nchi itarudi kwenye utawala mbovu. Chaguo ni la mama na dalili siyo nzuri kabisa mpaka sasa,” amedai. Lissu amesema pamoja na serikali kushindwa katika kesi iliyofunguliwa na Bob Wangwe kuhusu wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi, wakurugenzi hao wakizuiwa kusimamia uchaguzi na Mahakama ya Afrika hivi karibuni, hadi sasa hakujachukuliwa hatua zozote za kuwazuia kuendelea kusimamia uchaguzi kama ilivyoamriwa katika hukumu ya mahakama hiyo.

“Wanajua huwa wanashinda kwa namna gani, wanashinda kwa sababu tume siyo huru. Wakurugenzi wote ni wateule wa Rais. Wengi wao ni CCM kwa matendo yao na kwa kadi zao na tangu mwaka 1995 kumwekuwa na mapendekezo kuwa tume iwe na watumishi wake ambao watawajibika kwa tume moja kwa moja, hawa wakurugenzi wanawajibika kwa Rais, ni wateule wa Rais. Tume yenyewe ni wateule wa Rais.

“Kwa hiyo, mfumo huu usipobadilishwa kama ambavyo imependekezwa mara nyingi na kama ambavyo Mahakama ya Afrika sasa imeamua, maana yake ni kwamba tunajitafutia matatizo.”

**KIKOKOTOO MAFAO**

Kuhusu kikokotoo cha mafao ya wastaafu, kiongozi huyo wa CHADEMA amedai kikokotoo kipya kimeletwa ili kupoka wafanyakazi fedha zao.

Amesema kikokotoo hicho kimeletwa baada ya mifuko ya hifadhi ya jamii kufilisika kwa fedha zake kutumiwa vibaya, hivyo kukosekana fedha za kuwalipa wafanyakazi pindi wanapostaafu.

“Hizi fedha ambazo wafanyakazi wanachangia kila wanapolipwa mshahara, hizo hela zimechezewa sana kwa muda mrefu katika awamu zote. Ni mifuko ambayo haina uwezo wa kifedha kuwalipa wafanyakazi stahiki zao. Kwa hiyo, kikokotoo ni namna ya kutengeneza fomula ambayo itaonekana kama ni ya kisheria hivi.

“Fomula ambayo itaonekana kama ni halali hivi, lakini kimsingi ni namna ya kutekeleza... (alitamka neno linalohitaji uthibitisho kisheria). Fedha zimechezewa zimepelekwa katika miradi isiyokuwa na maana yoyote kwa wafanyakazi.”


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
05.07.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **10.07.2023 hadi 17.07.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB15200 / DS00TGGP / NRB43293**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 36.5 Upana - mita 4.30 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam kupitia Barabara ya Morogoro**, Barabara ya Mandela gari litasafiri muda wa mchana ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


# Mgogoro mpaka wa hifadhi watawala mazishi ya mbunge

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SAKATA la mgogoro wa mpaka kati ya wananchi na Hifadhi ya Taifa Ruaha, umetawala mazishi ya aliyekuwa Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, jana waliongoza maelfu ya wananchi kuaga mwili wa mbunge huyo kwenye viwanja vya polisi Kituo cha Chimala. Viongozi hao wawili pia hawakuacha kuzungumzia mgogoro huo.

Mtega ambaye alikuwa kinara wa kuwatetea wananchi katika mgogoro huo, alifariki dunia mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kugongwa na trekta (power tiller) katika eneo la Kibaoni, Kata ya Ihahi alipokuwa anaendesha pikipiki kuelekea shambani kwake.

Akitoa salamu za serikali, Waziri Mkuu Majaliwa alisema Mtega alikuwa anapigania haki za wananchi wa Mbarali hasa katika mgogoro huo wa mpaka baina yao na hifadhi. Alisema Mtega alikuwa anazungumza mara kwa mara katika vikao vya Bunge na kwenye vikao mbalimbali vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) namna mgogoro huo ulivyokuwa unaathiri maisha ya wananchi.

Alisema kuwa katika moja ya vikao vya Rais Samia Suluhu Hassan na wabunge wa CCM, Mtega alimshukuru Rais kwa kutuma timu ya mawaziri wanane wa kisekta kwa ajili ya kushughulikia mgogoro huo.

Alisema kuwa mbali na kushukuru, mbunge huyo pia aliomba maeneo zaidi yapunguzwe katika hifadhi na kurejeshwa kwa wananchi kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi.

“Maombi hayo ndiyo yaliyomfanya Mheshimiwa Rais kuondoa zaidi ya vijiji 34 ambavyo vilikuwa ndani ya hifadhi na akawaruhusu wananchi waendelee na shughuli zenu,” alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alisema mbunge huyo alikuwa anawashirikisha viongozi wa juu wa serikali kunapokuwa na tatizo lolote linalowakabili wananchi wake.

Mwakilishi wa wabunge wa vyama vya upinzani, Sophia Mwakagenda ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, alisema marehemu Mtega alikuwa mkweli na muwazi.

Alisema kiongozi huyo alikuwa anazungumza kwa ujasiri kama walivyo wabunge wa vyama vya upinzani, jambo ambalo lilikuwa linawapa faraja wabunge walio wachache kwa kujiona kwamba wana watu wengine wanaowaunga mkono.

“Kupitia Mtega iwe funzo kwa CCM kuchagua wabunge ambao wanafanya kazi kwa maslahi ya wananchi na siyo maslahi binafsi, ametumia muda wake aliokuwa bungeni kuwatetea wananchi wa Mbarali,” alisema Sophia.

Alisema kutokana na kutetea wananchi waliokuwa wanaathiriwa na GN 28 (mpaka wa hifadhi), baadhi ya wabunge walimbatiza jina la tangazo hilo na alikuwa anasimamia kile anachoamini kuwa ni haki ya wananchi.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Mikoa ya Mbeya na Songwe, Oran Njeza, alisema baada ya kumaliza vikao vya Bunge walikubaliana kufanya ziara katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbarali kwa lengo la kutatua kero za wananchi.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliwataka wananchi wa Jimbo la Mbarali kuendelea kuwa watulivu katika kipindi chote cha maombolezo ili msiba huo umalizike kwa amani na utulivu.




TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

**KUMB: PPR/2023 - 07/01**

# TAARIFA KWA UMMA

## BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 5 JULAI 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, tarehe 5 Julai 2023 saa 6:01 usiku. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za rejareja za mafuta ya petroli na dizeli yaliyopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam zimeshuka kwa shilingi 137/Lita na shilingi 118/lita, mtawalia, ikilinganishwa na bei za toleo la tarehe 7 Juni 2023. Pia, bei ya rejareja ya mafuta ya taa kwa Julai 2023 itaendelea kuwa ni ile iliyotangazwa katika toleo la tarehe 7 Juni 2023 kwa kuwa hakuna shehena iliyopokelewa mwezi Juni 2023.

(b) Kwa Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara), bei ya rejareja ya mafuta ya petroli imeshuka kwa Shilingi 188/Lita wakati bei ya mafuta ya dizeli imeongezeka kwa shilingi 58/lita ikilinganishwa na bei za toleo la tarehe 7 Juni 2023.

(c) Kwa Mikoa ya Kusini (Lindi, Mtwara, na Ruvuma), hakuna shehena ya bidhaa za mafuta iliyopokelewa kupitia Bandari ya Mtwara kwa Juni 2023. Hivyo basi, bei ya rejareja ya dizeli kwa mwezi Julai 2023 itaendelea kuwa ni ile iliyotangazwa katika toleo la tarehe 7 Juni 2023. Kutokana na upungufu wa bidhaa ya petroli katika maghala ya kuhifadhi mafuta yaliyopo Mtwara, waendeshaji wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Kusini wanashauriwa kuchukua mafuta hayo kutoka katika bandari ya Dar es Salaam. Hivyo basi, bei za rejareja za mafuta ya petroli katika mikoa hiyo zitazingatia bei kikomo ya rejareja ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.

(d) Aidha, kwa kuwa hakuna mafuta ya taa katika maghala yaliyopo katika Bandari za Tanga na Mtwara, waendeshaji wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Kaskazini na Kusini wanashauriwa kuchukua mafuta hayo kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo zitazingatia bei kikomo ya rejareja ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.

Bei za Mikoa, Wilaya na Miji, ni kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na. 1. Tofauti ya bei kutoka sehemu moja kwenda nyingine inatokana na tofauti ya bei ya mafuta katika bandari ambayo mafuta yamepakuliwa na gharama za usafirishaji.

Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za uagizaji (BPS Premium) na thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani.

Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

i. EWBei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
ii. Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
iii. Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap) au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama ilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 la tarehe 28 Januari 2022 na marekebisho ya Kanuni hii kama yalivyotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 421 la tarehe 23 Juni 2023.
iv. Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.
v. Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.
vi. Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 1. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.
vii. Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 2. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.

**JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA - SHILINGI/LITA**

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Dar es Salaam** | **2,736** | **2,544** | **2,829** |
| **Arusha** | **2,781** | **2,816** | **2,913** |
| Arumeru (Usa River) | 2,781 | 2,816 | 2,913 |
| Karatu | 2,799 | 2,835 | 2,931 |
| Longido | 2,792 | 2,827 | 2,924 |
| Monduli | 2,786 | 2,822 | 2,918 |
| Monduli-Makuyuni | 2,791 | 2,826 | 2,923 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,866 | 2,901 | 3,005 |
| **Coast (Kibaha)** | **2,741** | **2,548** | **2,833** |
| Bagamoyo | 2,747 | 2,555 | 2,840 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,778 | 2,586 | 2,871 |
| Bagamoyo (Mbwewe) | 2,759 | 2,567 | 2,852 |
| Chalinze Junction | 2,750 | 2,558 | 2,843 |
| Chalinze Township (Msata) | 2,755 | 2,562 | 2,847 |
| Kibiti | 2,757 | 2,564 | 2,849 |
| Kisarawe | 2,743 | 2,551 | 2,836 |
| Mkuranga | 2,746 | 2,554 | 2,839 |
| Rufiji | 2,764 | 2,571 | 2,857 |
| **Dodoma** | **2,795** | **2,603** | **2,888** |
| Bahi | 2,802 | 2,610 | 2,895 |
| Chamwino | 2,790 | 2,598 | 2,883 |
| Chemba | 2,822 | 2,629 | 2,914 |
| Kondoa | 2,828 | 2,635 | 2,921 |
| Kongwa | 2,792 | 2,600 | 2,885 |
| Mpwapwa | 2,796 | 2,604 | 2,889 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 2,808 | 2,616 | 2,901 |
| Mtera (Makatopora) | 2,814 | 2,622 | 2,907 |
| Mvumi | 2,802 | 2,609 | 2,894 |
| **Geita** | **2,902** | **2,709** | **2,994** |
| Bukombe | 2,891 | 2,698 | 2,983 |
| Chato | 2,923 | 2,730 | 3,015 |
| Mbogwe | 2,940 | 2,747 | 3,032 |
| Nyang'hwale | 2,917 | 2,724 | 3,009 |
| **Iringa** | **2,800** | **2,608** | **2,893** |
| Ismani | 2,806 | 2,613 | 2,898 |
| Kilolo | 2,805 | 2,612 | 2,897 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,810 | 2,618 | 2,903 |
| Mufindi (Igowole) | 2,819 | 2,627 | 2,912 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,952** | **2,759** | **3,044** |
| Biharamulo | 2,926 | 2,734 | 3,019 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,968 | 2,776 | 3,061 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,974 | 2,782 | 3,067 |
| Muleba | 2,952 | 2,759 | 3,044 |
| Ngara | 2,940 | 2,747 | 3,032 |
| Misenyi | 2,960 | 2,768 | 3,053 |
| **Katavi (Mpanda)** | **2,894** | **2,702** | **2,987** |
| Mlele (Inyonga) | 2,876 | 2,683 | 2,968 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,913 | 2,721 | 3,006 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,912 | 2,720 | 3,005 |
| **Kigoma** | **2,899** | **2,706** | **2,991** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,889 | 2,696 | 2,982 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 2,897 | 2,705 | 2,990 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 2,899 | 2,707 | 2,992 |
| Buhigwe | 2,897 | 2,705 | 2,990 |
| Kakonko | 2,899 | 2,707 | 2,992 |

TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kasulu | 2,908 | 2,715 | 3,000 |
| Kibondo | 2,905 | 2,713 | 2,998 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,771** | **2,806** | **2,903** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,774 | 2,809 | 2,906 |
| Mwanga | 2,764 | 2,799 | 2,896 |
| Rombo (Mkuu) | 2,787 | 2,823 | 2,924 |
| Same | 2,757 | 2,792 | 2,889 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,777 | 2,813 | 2,909 |
| **Lindi** | **2,795** | **3,013** | **2,888** |
| Lindi-Mtama | 2,813 | 3,018 | 2,906 |
| Kilwa Masoko | 2,770 | 3,037 | 2,863 |
| Liwale | 2,816 | 3,049 | 2,909 |
| Nachingwea | 2,824 | 3,033 | 2,917 |
| Ruangwa | 2,826 | 3,040 | 2,919 |
| **Manyara (Babati)** | **2,815** | **2,850** | **2,951** |
| Hanang (Katesh) | 2,826 | 2,861 | 2,962 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,830 | 2,866 | 2,962 |
| Mbulu | 2,828 | 2,863 | 2,964 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,847 | 2,882 | 2,983 |
| **Mara (Musoma)** | **2,902** | **2,710** | **2,995** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,915 | 2,722 | 3,007 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,909 | 2,717 | 3,002 |
| Rorya (Shirati) | 2,917 | 2,724 | 3,010 |
| Bunda | 2,893 | 2,701 | 2,986 |
| Bunda (Kisorya) | 2,906 | 2,713 | 2,998 |
| Butiama | 2,899 | 2,707 | 2,992 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,910 | 2,718 | 3,003 |
| Tarime | 2,911 | 2,718 | 3,003 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,916 | 2,724 | 3,009 |
| **Mbeya** | **2,843** | **2,651** | **2,936** |
| Chunya | 2,853 | 2,661 | 2,946 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,858 | 2,666 | 2,951 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 2,860 | 2,668 | 2,953 |
| Kyela | 2,859 | 2,667 | 2,952 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,828 | 2,635 | 2,920 |
| Rujewa (Madibira) | 2,841 | 2,648 | 2,933 |
| Rujewa (Kapunga) | 2,837 | 2,645 | 2,930 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,852 | 2,660 | 2,945 |
| Busokelo (Iwangwa) | 2,856 | 2,663 | 2,948 |
| **Morogoro** | **2,761** | **2,569** | **2,854** |
| Mikumi | 2,777 | 2,585 | 2,870 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,799 | 2,607 | 2,892 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,822 | 2,629 | 2,914 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,811 | 2,618 | 2,903 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,810 | 2,617 | 2,902 |
| Malinyi | 2,820 | 2,628 | 2,913 |
| Kilosa | 2,780 | 2,587 | 2,872 |
| Gairo | 2,780 | 2,587 | 2,872 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,772 | 2,579 | 2,864 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,761 | 2,569 | 2,854 |
| Turian | 2,786 | 2,594 | 2,879 |
| **Mtwara** | **2,809** | **3,000** | **2,901** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,858 | 3,036 | 2,950 |
| Masasi | 2,834 | 3,016 | 2,927 |
| Newala | 2,841 | 3,021 | 2,933 |
| Tandahimba | 2,834 | 3,014 | 2,927 |
| Nanyamba | 2,834 | 3,014 | 2,927 |
| **Mwanza** | **2,886** | **2,694** | **2,979** |
| Kwimba | 2,904 | 2,712 | 2,997 |
| Magu | 2,895 | 2,702 | 2,987 |
| Misungwi | 2,881 | 2,688 | 2,973 |
| Misungwi (Mbarika) | 2,891 | 2,699 | 2,984 |
| Sengerema | 2,919 | 2,726 | 3,012 |
| Ukerewe | 2,946 | 2,754 | 3,039 |
| **Njombe** | **2,829** | **2,636** | **2,921** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,849 | 2,657 | 2,942 |
| Ludewa | 2,867 | 2,674 | 2,959 |
| Makambako | 2,821 | 2,629 | 2,914 |
| Makete | 2,860 | 2,667 | 2,952 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,827 | 2,634 | 2,919 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,909** | **2,717** | **3,002** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,909 | 2,717 | 3,002 |
| Kalambo (Matai) | 2,916 | 2,724 | 3,009 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,923 | 2,730 | 3,015 |
| Nkasi (Kirando) | 2,932 | 2,740 | 3,025 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,860** | **3,085** | **2,952** |
| Mbinga | 2,872 | 3,098 | 2,965 |
| Namtumbo | 2,865 | 3,076 | 2,958 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,883 | 3,123 | 2,975 |
| Tunduru | 2,840 | 3,050 | 2,932 |
| **Shinyanga** | **2,865** | **2,673** | **2,958** |
| Kahama | 2,870 | 2,677 | 2,962 |
| Kishapu | 2,873 | 2,681 | 2,966 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,882 | 2,689 | 2,974 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 2,887 | 2,695 | 2,980 |
| Salawe | 2,879 | 2,687 | 2,972 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,883** | **2,691** | **2,976** |
| Busega (Nyashimo) | 2,895 | 2,703 | 2,988 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,883 | 2,691 | 2,976 |
| Maswa | 2,877 | 2,685 | 2,970 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,888 | 2,696 | 2,981 |
| **Singida** | **2,827** | **2,635** | **2,920** |
| Iramba | 2,839 | 2,647 | 2,932 |
| Manyoni | 2,812 | 2,619 | 2,904 |
| Itigi (Mitundu) | 2,827 | 2,635 | 2,920 |
| Ikungi | 2,823 | 2,630 | 2,915 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,852 | 2,659 | 2,944 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,853** | **2,660** | **2,945** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,860 | 2,667 | 2,952 |
| Ileje | 2,857 | 2,664 | 2,949 |
| Momba (Chitete) | 2,862 | 2,669 | 2,954 |
| Tunduma | 2,857 | 2,664 | 2,949 |
| **Tabora** | **2,845** | **2,652** | **2,937** |
| Igunga | 2,844 | 2,652 | 2,937 |
| Kaliua | 2,858 | 2,665 | 2,950 |
| Ulyankulu | 2,855 | 2,663 | 2,948 |
| Nzega | 2,855 | 2,662 | 2,948 |
| Sikonge | 2,853 | 2,661 | 2,946 |
| Urambo | 2,854 | 2,662 | 2,947 |
| Uyui | 2,851 | 2,658 | 2,943 |
| Mpyagula | 2,876 | 2,684 | 2,969 |
| **Tanga** | **2,724** | **2,760** | **2,875** |
| Handeni | 2,745 | 2,780 | 2,854 |
| Kilindi | 2,760 | 2,795 | 2,889 |
| Korogwe | 2,737 | 2,772 | 2,868 |
| Lushoto | 2,746 | 2,781 | 2,878 |
| Mkinga (Maramba) | 2,731 | 2,767 | 2,889 |
| Muheza | 2,729 | 2,765 | 2,875 |
| Pangani | 2,731 | 2,766 | 2,882 |

**JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA - SHILINGI/LITA**

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,605.74 | 2,413.53 | 2,698.35 |
| Tanga | 2,593.92 | 2,628.76 | - |
| Mtwara | 2,662.38 | 2,867.94 | - |

**Dkt. James A. Mwainyekule**
**MKURUGENZI MKUU- EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe kwa waliobaka na kumfunga katika kiroba mjamzito

**KUBAKA** ni kosa la jinai kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kanuni za Adhabu, Kifungu cha 130(1) na adhabu yake katika Kifungu cha 131(1) cha sheria hiyo ambayo ni kifungo cha maisha gerezani, ikiambatana na adhabu ya viboko na faini.

Katika toleo letu la Jumatatu ya juma hili, tulichapisha ripoti ya uchunguzi kuhusu tukio la mjamzito kubakwa.

Ni uhalifu uliofanywa usiku wa saa za kulala - saa nne usiku Juni 5 mwaka huu, katika Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

Leo unatimu mwezi mzima tangu tukio hili. Pamoja na maelezo ya mtoto aliyeshuhudia unyama dhidi ya mama yake, maelezo ya mama, majirani, askari walinzi wa usiku (sungusungu) na vielelezo kadhaa vinavyoweza kuibua nani wanaweza kuwa watenda unyama kwa mjamzito, polisi hawajakamata hata mtuhumiwa mmoja.

Pia kuna shida nyingine - mjamzito huyo alipofikishwa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, anadai kutojazwa kwa wakati Fomu Na. 3 ya Polisi (PF3), pia kupewa vidonge vya kuzuia maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) pasi na maelekezo, akazitupa shambani.

Ni madai ambayo Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani imeahidi kuyafanyia uchunguzi ili kubaini ukweli wake.

Wakati ofisi hiyo ikichukua uamuzi huo, tayari wadau wa haki za binadamu na ustawi wa makundi maalum, kikiwamo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) wamelaani ukatili dhidi ya mjamzito huyo, wakitaka hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Nipashe, tukiwa wadau wa haki za binadamu na wafuatiliaji wa utekelezaji wa sera na mipango ya serikali, tunaungana na wadau wengine kulaani kitendo hicho cha kikatili dhidi ya mjamzito huyo.

Na kwa kuwa Jeshi la Polisi kupitia kwa Kamanda wake wa Mkoa wa Kipolisi Rufiji limekiri kuwa na taarifa za uhalifu huo, likishikilia pikipiki inayodaiwa kutelekezwa eneo la tukio, pia kutuma ofisa wake wa Dawati wa Jinsia kuzungumza na mjamzito huo, Nipashe tunashauri hatua zichukuliwe dhidi ya waliotenda ukatili huo ili haki itendeke kwa mujibu wa sheria.

Ukatili dhidi ya mjamzito huyo si tu kwamba unakiuka sheria tajwa hapo juu, bali pia unakiuka Katiba ya nchi, inayoelekeza kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake.


Katiba ya nchi inaielekeza serikali kuweka utaratibu wa sheria kulinda haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake.

Uhalifu uliofanywa dhidi ya mjamzito huyo, unakinzana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia Tanzania ya Mwaka 2000 inayolenga kuweka mazingira wezeshi, kutatua vikwazo dhidi ya wanawake na kuleta haki na usawa ili kundi hilo lishiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika programu na miradi ya maendeleo.

Pia ni kitendo kinachokwaza utekelezaji wa Lengo Na. 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha zinatilia mkazo usawa wa kijinsia.

Tanzania pia imeshatia saini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mwaka 1979, unaoelekeza kuondoa aina zote za ubaguzi na uonevu kwa wanawake. Shime, hatua zichukuliwe!

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Wanawake tumieni umoja kupata 50/50

**LINAPOKUJA** suala la usawa wa kijinsia katika uongozi na majukumu mengine, wanawake wapo mstari wa mbele kulipigania ili kupata usawa huo unakuwapo kati yao na wanaume.

Hiyo ni katika kushika nafasi mbalimbali za uongozi, zikiwamo za kuchaguliwa au kuteuliwa, kwani wanaamini kwamba uongozi hauna jinsi, awe mwanaume au mwanamke, wote wanaweza kupewa jukumu liwe la kiuteuzi au kupigiwa kura.

Vilevile wanatambua kuwa uongozi si kutumia misuli bali ni elimu, weledi, hekima na busara, hivyo watetezi wa harakati wa jinsia wamekuwa wakijitahidi kuelimisha umma wa Watanzania

Kutokana na hatua hiyo ya kuelimisha umma wa Watanzania, zipo juhudi mbalimbali ambazo zimechukuliwa za kuhakikisha usawa kijinsia unazingatiwa kwenye uongozi na maeneo mengine.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ni miongoni mwa watetezi hao ambacho kinasema tangu mwaka 1997, Tanzania imeshuhudia mabadiliko hayo ikiwamo uteuzi.

Kwa mujibu wa kituo hicho, ni kwamba kumekuwapo na mambo chanya mbalimbali kwenye masuala ya uongozi na mipango madhubuti yanayolenga kufikia usawa wa kijinsia.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, katika ufafanuzi wake anasema kwa sasa mabalozi wanawake wanaoiwakilisha Tanzania mataifa mbalimbali ni zaidi ya tisa dhidi ya 33.

Aidha, wakuu wa mikoa ni zaidi ya sita dhidi ya 20, wakuu wa wilaya zaidi 40 kati ya 101.

Anasema yapo maeneo mengi ambayo anataja kuwa kuna hatua kubwa na mafanikio kuelekea 50/ 50 akiongoza kuwa ni kazi nzuri ambayo Tanzania inaelekea kuanzia mwaka 1977 hadi 2023.

Pia anaongeza kuwa kumekuwapo na mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazolinda na kutetea haki za wanawake ikiwamo kuweka wizara mahsusi kwa masuala ya jinsia, hali inayoonyesha kuwa usawa wa kijinsia unapewa umuhimu.

Pamoja na hayo, kuna msemo usemao, ukishikwa shikamana. Hivyo ingekuwa ni vyema wakati serikali inawashika, basi nao washikamane bila kujali itikadi za vyama wanavyotoka.

Mara nyingi imekuwa ni kawaida kwa wanasiasa kuegemea kwenye itikadi za vyama vyao hata kwa mambo ya msingi yenye lengo la kuwaunganisha bila kujali ni wanawake, vijana au wapigakura.

Hivyo, kwa kuwa wanakiri kwamba serikali imeanza kuchukua hatua za kuleta usawa wa kijinsia, basi ni vyema nao wakaleta usawa kwa kutobaguana kutokana na itikadi za vyama.

Wao wenyewe wamekuwa wakikiri kwamba wanakumbana na vikwazo vingi kutoka kwa wanaume wanapotafuta uongozi katika vyama, lakini ajabu wanapokutana kwenye majukwaa yao wakitokea katika vyama tofauti vya siasa, idaiwa kuwa nao hubaguana.

Ninadhani ukatili wa kijinsia ambao wamekuwa wakikutana nao ungeweza kuwaunganisha na kuwa na kuwa lugha moja wanapotafuta usawa wa kijinsia ili hatimaye 50 kwa 50 iweze kutimia.

Mwaka kesho kuna uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, ingekuwa ni vyama kama wanawake wataanza kujipanga sasa kwa kuwaandaa wagombea badala ya kuwa wapigakura tu.

Kuna msemo kwamba 'wanawake ni jeshi kubwa', jeshi hilo liamke lijitambue na litumike kuhakikisha wanapata nafasi nyingi za uongozi bila kujali itikadi za vyama, ukanda, hali ya uchumi au elimu na chochote vinginevyo wanaweza kuendelea kuwa wapigakura badala kugombea na kuchaguliwa.

Ninaamini kupitia wingi wao usiobagua itikadi za vyama, unaweza kuwafikisha mbali katika harakati zao za kutafuta usawa wa kijinsia, hivyo, ingefaa walitafakari hilo na kulifanyia kazi.

Kinamama wanaweza, kauli mbiu hiyo ianze kwa wenyewe kwa wenyewe kuunganana, kushirikiana na kuinuana kwa hali yoyote nje na ndani ya jukwaa la kisiasa.

# Mabula ataka usimamizi mzuri katika miradi ya maendeleo

**Na Munir Shemweta**

MBUNGE wa Ilemela ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, ameagiza kuwapo usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika jimbo hilo la mkoani Mwanza.

Dk. Mabula aliagiza hayo jana jijini Mwanza katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa jimboni.

Alisisitiza umuhimu wa matumizi thabiti ya fedha za maendeleo sambamba na uzalendo katika utekelezaji wa miradi.



"Ni vizuri wakati wa utekelezaji miradi katika Jimbo la Ilemela mkahakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha za maendeleo lakini pia uzalendo uwekwe mbele," aliagiza.

Dk. Mabula alikagua wa miradi katika Kata ya Bugogwa - Shule ya Msingi Igombe ambayo serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 69.1 kupitia Mradi wa Boost uliofanikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa shuleni huko sambamba na ujenzi wa shule mpya ya msingi katika Kata ya Kahama inayojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 540.3.

Waziri huyo pia alikagua wa ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Buswelu inayojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 540.3.

Maeneo mengine aliyotembelea ni pamoja na mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum linalojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 100 katika Shule ya Msingi Buswelu na zahanati mpya iliyojengwa Kata ya Ilemela, Mtaa wa Lumala ambayo zaidi ya Sh. milioni 142 zimetumika huku mbunge huyo akichangia matofali zaidi 3,500.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Ilemela, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilemela, Hassan Milanga, alisema chama kinatambua jitihada za mbunge katika kuwatumikia wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, aliishukuru serikali kwa kuipatia Ilemela fedha nyingi za miradi ambazo zinakwenda kutatua changamoto mbalimbali wilayani mwake.

Akihitimisha ziara hiyo, Waziri Mabula alitoa wito kwa wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi ya maendeleo anayoifanya.

# TRA yatangaza makusanyo ya 2022/23

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema katika mwaka uliopita wa fedha (2022/23), ilikusanya Sh. trilioni 24.11 sawa na ufanisi wa asilimia 97.4 ya lengo la makusanyo ya Sh. trilioni 24.76.

TRA imesema makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 8.2 kulinganishwa na ya mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa mujibu wa taarifa ya mamlaka hiyo iliyotolewa juzi na kutiwa saini na Kamishna Mkuu, Alphayo Kidata, katika robo ya mwaka wa fedha 2022/23 (Aprili hadi Juni), TRA ilikusanya Sh. trilioni 5.69 sawa na ufanisi wa asilimia 91.1 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 6.24.

"Makusanyo haya ni sawa na ongezeko la asilimia 1.6 kulinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Kwa namna ya pekee kabisa, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa serikali kwa kuendelea kuiwezesha TRA katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kiutendaji," alisema.

Kamishna Kidata alisema serikali imeendelea kuiwezesha TRA katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuboresha ufanisi katika utekelezaji majukumu ya makusanyo.

Aliyataja maboresho hayo kuwa ni ujenzi na uboreshaji wa mifumo ya ukusanyaji mapato, uboreshaji wa mazingira ya kufanya kazi na vitendea kazi na kuongeza watumishi wapya.

Alisema hatua hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa utendaji kazi. Kwa huu wa fedha, mamlaka inatoa rai kwa walipakodi na wananchi kuhakikisha wanatoa risiti sahihi za kielektroniki katika kila mauzo wanayofanya na wanunuzi wadai risiti sahihi.

"Walipakodi wawasilishe ritani sahihi, kulipa kodi stahiki na kulipa madeni ya kodi kwa hiari na kwa wakati uliowekwa kisheria ili kuepukana na riba na adhabu zisizo za lazima.

"Wazalishaji na waingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa, wazingatie matumizi sahihi ya stempu za ushuru wa bidhaa na walipakodi na wadau waendelee kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na mamlaka kuhusu elimu ya kodi na matumizi ya mifumo ya usimamizi wa kodi," alisema.

# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 343 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 20/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | 1.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.59847 KIWANJA NA.2009 KITALU "D" | 1.LAMECK JOHN RUGIGA 2.CRISPIN PATRICK KAPILIMBA | 1.MBEZI MSHIKAMANO 2.SINZA | 18/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 11/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MAGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 12/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 13/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FELISTA MATOKE NYAGWE | NYUMBA YENYE HATI NA.45634,KIWANJA NA.183 KITALU 'B' | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 13/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 14/07/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | NYUMBA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | GEITA | 26/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SONGALELI SAMA MZEE | KIWANJA | SONGALELI SAMA MZEE | BUSWELU MWANZA | 12/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 12/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 14/07/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAPPINESS NYANDA MAYALA | NYUMBA YENYE HATI NA. 99009, KIWANJA NA."9" KITALU " F" | SAIDI NYANDA MAYALA | IGOMA MWANZA | 22/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | T/A NINIGANI DEPOT EDWARD | NYUMBA | EDWARD JEREMIA MASSASI | MIHAMA BWIRU | 20/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ALEXANDER STANSLAUS NTAKILE | NYUMBA | ALEXANDER STANSLAUS NTAKILE | BUZURUGA NYAKATO | 22/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | BUS TATA T847 DKN | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | MWANZA MJINI | 20/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'O10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.CHAMAZI DOVYA | 17/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.175184 KIWANJA NA.1370 KITALU "A" | KASSIAN ANTON NINDI | TABATA KISUKULU | 26/07/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 19/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 14/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA (2) ZENYE HATI YA MAUZIANO | 1.FRENK SAMSON LEMAU 2.MARIAM PETER NGAJILO | SHEWA-MBEYA | 25/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 13/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 12/07/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | GERALD VENANCE SALLEH | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.85778 KIWANJA NA.2166 KITALU "B" MBEZI LUIS | GERALD VENANCE | MBEZI LUIS | 22/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 19/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | SABRINA ALLY MZEE | NYUMBA | SABRINA ALLY MZEE | KIPAWA | 19/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | NYUMBA | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | KINYEREZI | 24/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | KASOGA NETTO MATOME | NYUMBA | KASOGA NETTO MATOME | KIPAWA | 24/07/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | WANSAGULA MOSES NATUMWA | NYUMBA | PILI HARUNA BUHANGWA | PUGU- KINYAMWEZI | 20/07/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ELIZABETH PHILIPO CHIWILI | NYUMBA | ELIZABETH PHILIPO CHIWILI | KITUNDA KATI, ILALA | 20/07/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0787129539/0745707008/0743885084/0655715138/0692836202
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# FCC yafuatilia kuumizana kibiashara

Na Maulid Mmbaga

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya Ushindani (FCC), Willium Erio, amesema wanahakikisha wanaoshiriki katika ushindani wa biashara, wanafanya hivyo bila kuumizana au kufanya vurugu zinazowafanya wengine washindwe kuendesha shughuli zao.

Katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam, Erio aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa wajibu mkubwa wa tume hiyo ni kuhakikisha wanalinda ushindani.

Pia alisema wanahakikisha wanaofanya biashara, wanafanya hivyo kwa kuzingatia misingi ya shughuli hizo na hawapati vikwazo vyovyote vitakavyowafanya washindwe kufanya biashara zao vizuri.

"Tunawezesha kampuni ambazo zinataka kuja kufanya biashara katika nchi yetu kwa kuzingatia misingi iliyopo kwa sababu kuna njia nyingi za kufanya biashara katika eneo au nchi kuanzisha kampuni au kuungana na kampuni zingine.

"Kazi yetu ni kuhakikisha tunafanya tathmini ya kitaalamu na kuhakikisha muungano ule wa kampuni hauleti athari kwa watu wengine wala katika uchumi wa nchi yetu," alisema Erio.

Alisema huwezesha kampuni kukua kibiashara na kuendesha shughuli za kiuchumi kwa utaratibu ambao utakuwa ni rahisi kwao, ikiwamo kuwaunganisha na watu wenye mitaji na watakaowaongeza elimu na uelewa katika uendeshaji wa biashara.

"Kwa mfano, huwezi kuingia mkataba na benki ambao una kifungu kinachosema mkopeshaji ana haki ya kubadilisha kiwango cha riba wakati wowote. Kuweka masharti ambayo yako katika lugha ya kigeni peke yake kiasi kwamba watu wetu hawaelewi na kuwa na maandishi madogo yasiyosomeka.

"Mikataba yote tunaipitia na kuhakikisha kwamba iko sawa, ndiyo watu waipitishe na kuhakikisha yanayojiri wakati wa utekelezaji yanaendana na kile kilichopo katika mkataba. Pia tumekuwa tunahakikisha bidhaa bandia haziingii na kuuzwa nchini," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Roida Andusamile (kushoto), akikabidhi cheti cha jina la biashara kwa Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa Bodi ya Utalii, Augustina Makoye, katika Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA:JUMANNE JUMA**

# Mzumbe yaja na mfumo wa kudhibiti watoto kupotea

Na Beatrice Shayo

CHUO Kikuu cha Mzumbe kimetengeneza mfumo kwa ajili ya kudhibiti matukio ya watoto kupotea.

Mtoto akiwa katika eneo hatarishi, mzazi au mlezi atapata taarifa ya mlio wa kengele katika simu yake.

Mwanafunzi wa chuo hicho, Frank Msonge, ambaye ni miongoni mwa walioshiriki kutengeneza mfumo huo, alifafanua namna unavyofanya kazi, alipozungumza na mwandishi jana katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) mkoani Dar es Salaam.

Msonge alisema mfumo huo ni kwa ajili ya kumwongoza mtoto anapokuwa katika mazingira ambayo siyo salama kama vile nje ya nyumba au katika msongamano wa watu.

Mwanafunzi huo alisema kifaa hicho pia ni kwa ajili watu ambao wana mahitaji maalum, kinaweza kutumika kuwadhibiti popote wanapokuwa kupitia mzazi au mlezi.

"Mfano wazee au wale wenye matatizo ya akili anaweza kutumia kifaa hiki. Mfumo huu tumetengeneza kwa kuangalia teknolojia, hiki kifaa atavalishwa mtoto kama saa na kuweka umbali ambao mzazi anataka mtoto wake awapo hata mita 10.

"Kama nyumba ina geti labda hutaki mtoto aende nje ya geti, utamvalisha mtoto wako kifaa hiki na kuweka umbali unaotaka, akivuka huo umbali mzazi utapata taarifa kupitia mlio wa kengele katika simu yako ya kiganjani," alisema.

Mwanafunzi huyo alisema endapo mzazi amekwenda katika maonesho hayo na mtoto anaweza kumvalisha kifaa hicho na kuweka umbali wa kilometa 10 na anapozidisha atakapa taarifa.

Msonge alisema lengo la kutengeneza mfumo huo ni kuzuia matukio ya watoto kupotea aliyoyataja yamekithiri nchini.

Hiki kifaa unaweza kubaini mtoto umbali wa mita 100 na vipo vya aina tofauti tofauti kulingana na mahitaji ya mtu. Vipo vyenye umbali zaidi ya huo, lengo la uangalizi mzazi anaweka umbali ambao anaona ni salama kuwapo kwa mtoto," alisema.

Mwanafunzi huyo alisema kwa sasa wapo katika hatua za mwisho za utengenezaji wa mfumo huo na ukikamilika utauzwa kwa bei zitazopendekezwa na chuo.

## TTCL kuwa mhimili uhifadhi takwimu za wafanyabiashara

Na Beatrice Shayo

MWENYEKITI wa Bodi wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Zuhura Muro, amesema shirika hilo linaweza kuwa mhimili mkubwa wa kuhifadhi takwimu za wafanyabiashara wakubwa na kati na kuwa salama wakati wowote.

Alibainisha hayo jana alipozungumza na mwandishi katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Zuhura alisema taarifa hizo zitakuwa katika kituo chao cha takwimu ambacho kimeunganishwa na vituo vyao vyote vilivyopo nchini.

Alisema kwa ushirikiano mzuri walionao na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), watahakikisha takwimu za wateja wao zitakwenda vizuri na nishati hiyo haitakosekana ili kila mmoja azipate inapotokea anazihitaji.

Alisema wameweka nguvu kubwa katika mkongo ambao utasaidia kupunguza gharama za mawasiliano na kuifanya nchi kuwa na miingiliano yenye tija zaidi na kuwezesha uchumi kuongezeka.

Zuhura alisema katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, TTCL itaisimamisha Tanzania kama kiongozi wa ukanda huo kwa kuziunganisha nchi ambazo hazina nafasi ya kufikia Bahari ya Hindi kuungamishwa kupitia digitali.

"Kwa njia hiyo, tutaongeza pato la fedha za kigeni, tutauza ubunifu wetu, tutauza teknolojia nje ya nchi kupitia TTCL. Shirika hili lina uwezo wa kuifanya Tanzania ikawa nchi kiongozi siyo tu kiteknolojia na kiuchumi katika ukanda wetu, bali pia kiusalama na kiutamaduni," alisema.

Zuhura alisema wanatoa huduma ya call centre (Kituo cha Mawasiliano cha Pamoja) kwa ajili ya mashirika mbalimbali.

"Badala ya wafanyabiashara au mashirika tunaandaa call centre zao, tuna uwezo huo kwa sababu tuna majengo, teknolojia na wataalamu wa kuendesha call centre. Kama una hospitali yako ya binafsi, shirika lako la bima, shirika la usafiri unaweza ukawa na Call Centre inayoendeshwa na TTCL," alibainisha.

Mkurugenzi wa Mkuu TTCL, Peter Ulanga, alisema wamekabidhiwa kuendesha mkongo wa taifa ambao unaunganisha nchi saba na kwa sasa wana mpango wa kuiunganisha Kongo ya Mashariki.

# DC azionya NGO zinazotoa taarifa za uongo za miradi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, Emmanuela Kaganda, ametoa onyo kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yanayotoa taarifa za uongo ikiwamo za udanganyifu wa mapato na matumizi ya fedha wanazotumia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Amesema serikali itazichukulia hatua kali za kisheria taasisi na mashirika hayo ikiwamo kuzifutia usajili kwa kuwa zitakuwa zimekwenda kinyume na sheria, kanuni na utaratibu.

Alitoa onyo hilo jana wakati wa kikao cha jukwaa la mashirika yasiyokuwa ya kiserikali katika Halmashauri ya Meru wilayani humo. Kaganda alisema wilaya hiyo itafanya msako wa kuyabaini mashirika yanayofanya kazi kinyume na utaratibu, pia yasiyokuwa na tija kwa jamii kwa kuwa yanakwamisha lengo la serikali ya kupeleka maendeleo kwa wananchi kwa wakati.

Pia ameyataka mashirika yote kwenye eneo hilo yanayofanya udanganyifu pamoja na ubadhirifu wa fedha za miradi kutoka kwa wahisani kuacha mara moja, huku akiagiza halmashauri hiyo kufuatilia kujua bajeti na shughuli zinazofanywa na mashirika hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Zainabu Makwinya, alisema utambuzi wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali unaendelea.

Mwenyekiti wa mashirika yasiyo ya serikali, Vicent Uhega, alisema mashirika hayo yataendelea kushirikiana na serikali kwa uwazi na ukaribu ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.



Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) mkoani Arusha, Amani Mwakalebela (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha jana, kuhusu mamlaka hiyo kusitisha mgomo wa daladala. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Daktari Bingwa: Maziwa ya ng'ombe ni hatari kwa watoto

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya watoto kutoka Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, Dk. Michael Irira, amesema matumizi ya maziwa ya ng'ombe kwa watoto wenye umri kati ya miaka miwili hadi mitatu ni hatari kwa afya zao, yanaweza kuwasababishia matatizo ya kiafya.

Alitoa kauli hiyo juzi wilayani Babati mkoani Manyara wakati akizungumza katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, kwenye kambi ya madaktari bingwa wa mama Samia kwa Kanda ya Kaskazini.

Awali alisema watoto waliowahudumia kwenye kambi hiyo alibaini wako wenye tatizo la utapiamlo, ukosefu wa madini ya chokaa, nimonia, kuharisha na wenye matatizo kwenye mfumo wa mkojo.

"Wanaotumia maziwa ya ng'ombe wanakosa madini ya chokaa kwa kuwa hayako kwenye maziwa ya ng'ombe," alisema Dk. Irira.

Aidha, alisema maziwa hayo siyo mazuri na ni vizuri mtoto asiyatumie mpaka atakapofikisha umri wa miaka miwili au mitatu kwa kuwa yanaweza kumletea madhara baadaye.

Alisema kuliko kutumia maziwa ya ng'ombe hayo ni bora mama akampa mtoto wake maziwa ya kopo kwa kuwa ni mazuri, ila mtoto awe ameishanyonya maziwa ya mama kwa muda wa miezi sita mfululizo bila kutumia kitu chochote.

Hata hivyo, alisema madini ya chokaa yako kwenye samaki na nyama ya ng'ombe hivyo watoto wasipopata kitoweo hicho, kwa kiasi cha kutosha watapata tatizo la kukosa madini hayo.

"Watoto wengi niliowahudumia kwa kiasi wana tatizo la ukosefu wa madini ya chokaa na wameishaonyesha dalili na wengine wana utapiamlo na wako chini ya miaka mitano," alisema.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) 2021/22-2025/26, inaelekeza lishe ya vyakula mchanganyiko na vya ziada kwa miezi sita mpaka 23 vimepewa kipaumbele zaidi wakati huo.

Kundi la umri wa miaka mitatu mpaka mitano linaendelea kupata huduma nyingine za lishe kama ufuatiliaji wa ukuaji, nyongeza ya Vitamin A, vidonge vya minyoo na usimamizi jumuishi wa magonjwa ya watoto.

Mkazi wa Kijiji cha Managha, Neema John, alisema alikuwa hajui kuwa maziwa ya ng'ombe yana madhara kwa watoto hivyo aliiomba serikali kuwapa elimu wazazi.

## TSB yawapa elimu, fursa wanawake Wakatoliki

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mkonge Tanzania (TSB), imetoa elimu ya kilimo cha mkonge, masoko na fursa zitokanazo na zao hilo kwa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA).

Elimu hiyo ilitolewa katika semina ya kuhitimisha kongamano la WAWATA Kanda ya Mashariki jijini Tanga.


Akizungumza kwenye semina hiyo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mkonge na Masoko wa TSB, Olivo Mtung'e, alisema bodi hiyo ambayo pia ni mdhamini wa kongamano hilo, imeona ni vema kuwashirikisha wanawake Wakatoliki kwenye katika suala zima la kuinua kipato chao na kujiimarisha kwenye familia kwa sababu wao ndiyo wasimamizi wa familia.

"Kama tunavyofahamu mkonge ni zao ambalo linavumilia sana ukame hasa ukizingatia sasa hivi tunapambana na hili tatizo la mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa Kanisa Katoliki wao walishaanza tangu mwaka 2015 kuzungumzia jambo hili ambapo Papa Francis alitoa waraka unaozunguzmia namna ya kukabiliana na changamoto hii ya mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Mtung'e alisema lengo la kuwakaribisha WAWATA kwenye kilimo kwa maana hiyo ya faida hizo zilizotajwa kwamba unaweza ukawa ni uzio au mpaka, lakini mkonge wenyewe unarutubisha ardhi.

"Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan amefungua nchi, yeye amefungua nchi kwa mataifa mbalimbali kupitia filamu yake ya Royal Tour sasa watalii wanakuja. Ukiangalia mkonge na bidhaa zake ni za asili kwa hiyo wenzetu wanaokuja kutoka mataifa mbalimbali wanategemea waje Afrika ambako watapata vitu vya asili," alisema.

Katibu wa Kamati ya Maandalizi ya Kongamano la WAWATA, Kanda ya Mashariki, Theodora Mtegeta, alisema Bodi ya Mkonge Tanzania ni mkombozi wa mwanamke ikiwa kama kikundi au mmoja mmoja na kuongeza kuwa hata yeye ni shahidi ambapo ana shamba amelima mkonge hivyo anajua namna hela ya zao hilo ilivyo tamu.



# Wachimbaji wakabidhi zahanati, gari la wagonjwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI zaidi ya 4,970 wa Kijiji cha Nyamishiga Kata ya Lunguya Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za matibabu baada ya wachimbaji wadogo wanawake kujenga zahanati.

Pia walikabidhi gari la wagonjwa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 312.53.

Akipokea msaada huo juzi, Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alikipongeza kikundi hicho kwa kukusanya maduhuli ya serikali zaidi ya Sh. bilioni mbili pamoja na msaada huo kama sehemu ya kurejesha kwa jamii akisema hali itakayosaidia kupunguza vifo.

Alisema kwa sasa wanaendelea kukamilisha taratibu za kisheria ili kikundi hicho kiweze kukabidhiwa leseni ya uchimbaji na kwa kile walichofanya kila rashi itakayopatikana watakuwa wanavipatia vikundi vya wanawake kwa sababu vinafanya mambo makubwa kulinganisha na vikundi vya kinababa.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema serikali mkoani humo itaendelea kushirikina na wadau wa afya katika kusogeza huduma karibu na wananchi.

Alisema Mkoa wa Shinyanga umepokea Sh. bilioni 26 za kuboresha huduma katika sekta ya afya na sasa dawa zinapatikana kwa asilimia 90 katika zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Alisema zahanati hiyo itaanza kutoa huduma mara moja ili kuwaondolea adha wananchi, wachimbaji kutembea umbali mrefu kupata huduma ya afya.

Akitoa taarifa ya kituo hicho, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lunguya, Teddy Jacob, alisema kituo hicho kilianza kujengwa na wananchi mwaka 2018 na kupata Sh. milioni 23.53 na kujenga boma lake.

Alisema fedha hizo zilichangwa kupitia mfuko wa sungusungu na zimetumika kukamilisha boma la kutolewa huduma wagonjwa wa nje mpaka wachimbaji hao walipokamilisha ujenzi.

Jacob alisema walipokea Sh. milioni 210 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo hilo kati ya hizo Sh. milioni 198.5 zilitumika kukamilisha ujenzi, kujenga vyoo vya kisasa, kichomea taka, nyumba ya mganga na kujenga mfumo wa kuvuna maji ya mvua ambayo yatakuwa yakitumika kituo hapo hasa kwa wajawazito wakati wa kujifungua. Aidha, alisema ukosefu wa zahanati kijijini hapo kiliwalazimu wananchi kutembea umbali wa kilometa 10 hadi Kituo cha Afya Lunguya kutafuta matibabu.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Mshikamano Mining Group, Semeni Malale, alisema, licha ya kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo wamekabidhi gari la wagonjwa lenye thamani ya Sh. milioni 75.



Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko (wa pili kulia), akikabidhi funguo ya gari la wagonjwa lenye thamani ya Sh. milioni 75 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Hamisi Katimba, lililotolewa na wachimbaji wadogo wanawake wa Nyamishiga, mkoani Shinyanga juzi, kwa ajili ya Zahanati ya Kijiji cha Nyamishiga. Wengine ni Mkuu wa mkoa huo, Christina Mndema (kulia) na (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Polisi wapewa mafunzo ya utayari kupambana na uhalifu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ASKARI polisi mkoani Shinyanga wamepewa mafunzo ya utayari ambayo yamelenga kuwajengea ukakamavu ili kufanya kazi zao kwa weledi na uadilifu katika kupambana na wahalifu.

Mafunzo hayo yamechukua muda wa miezi miwili na kuhitimishwa juzi na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mafunzo hayo, Kamanda Magomi alisema yametolewa kwa awamu ya kwanza kwa askari polisi ambao ni wakaguzi na wasaidizi wao.

Alisema mafunzo kama hayo yatatolewa tena kwa awamu ya pili yakiwa na lengo la kuwajengea uwezo wa utayari katika kukabiliana na uhalifu na kudumisha utulivu na amani.

"Mafunzo haya ni mwendelezo wa ratiba ya kawaida kwa askari wa vyeo mbalimbali ndani ya Jeshi la Polisi, miongoni mwa mafunzo mbalimbali yaliyotolewa ni pamoja na gwaride la heshima, pamoja na kufunga na kufungua silaha," alisema Kamanda Magomi.

Alisema pia yalitolewa mafunzo ya darasani katika masomo ya sheria, sayansi ya jinai, usalama barabarani, huduma ya kwanza, polisi jamii, rushwa, afya ya akili na masomo ya ulinzi wa mipaka kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Katika hatua nyingine Kamanda Magomi, aliwataka wakaguzi hao kwenda kutumia ujuzi walioupata kwenye mafunzo hayo kwa ajili ya manufaa ya wananchi, ili kuleta tija na kujenga imani kwa wananchi hao kwa kulinda usalama wao na mali zao.

# Jamii yapewa jukumu kudhibiti taka za plastiki

**Na Pelusy Yohana,** SAUT

JAMII imetakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tatizo la uchafuzi wa mazingira hususani wa taka za plastiki unadhibitiwa ili kuweka mazingira salama kwa viumbe hai waishio majini na nchi kavu.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Mazingira Wilaya ya Nyamagana, Sholi Maduhu, wakati akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu.

Alisema kila mtu anaweza kuchukua hatua ili kupunguza matumizi ya plastiki ambazo zimegeuka janga katika mazingira.

Alisema kuwa athari hasi za taka hizo katika Wilaya ya Nyamagana ni kubwa kulinganisha na faida zake kwani zimekuwa zikitupwa ovyo katika vyanzo vya maji pamoja na mazingira, kwamba husababisha madhara kwa mifugo.

"Kama jamii kuna hatua ambazo tunaweza kuchukua ili kupunguza kiwango cha uchafuzi wa plastiki katika maji, ikiwa ni pamoja kuchakata, kupunguza matumizi ya bidhaa za plastiki na kutumia chupa za maji zinazoweza kutumika tena ni njia zote za kusaidia kupambana na tatizo hili linaloongezeka na siyo kuwa na matumizi yasiyo ya muhimu ya bidhaa hizo."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Silivin, Ramadhan Malugu, alisema kuwa jamii inahitaji kuchukua hatua za haraka kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kuacha tabia za kupuuza tatizo na kuiachia serikali na wadau pekee jukumu hilo bali kila mmoja awe sehemu ya kudhibiti uchafuzi huo.

Aliongeza kuwa athari za plastiki kwa mazingira zimetambuliwa kama suala kubwa na kwa bahati mbaya tatizo hilo haliishii tu kwenye ardhi vilevile katika maji.

Kwa mujibu wa ripoti ya Jukwaa la Uchumi Duniani, ifikapo mwaka 2050, kiwango cha plastiki baharini kitazidi idadi ya samaki.

Pia inaelezwa kuwa tani milioni nane za plastiki hutupwa baharini kila mwaka.

James Lihepa ni mvuvi kutoka Mtaa wa Mswahili alisema kuwa matumizi ya chupa za plastiki yanachangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa samaki, kwamba wengi hukimbilia katika kina kirefu huku mazalia yakiharibiwa na taka hizo.



Ukurasa 12

**Wafuatiliaji watafuta sababu wazungumzaji Kiswahili kuongezeka kufikia milioni 500**




Ukurasa 13


Waambiwa tafuteni mbinu za kuingia ulingoni kutoka kwa watangulizi wenu

# siasa

JUMATANO JULAI 5, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

**DK. OMAR ALLY JUMA Makamu wa Rais wa kwanza, ndani ya vyama vingi, juhudi, kazi alizoasisi bado zinang'ara**

# Wadau wanavyoshangilia kuengua wakurugenzi kusimamia uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

KILA uchaguzi unapofanyika, umekuwa ukiambatana na malalamiko kutoka kwa baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani wakielekeza lawama zao kwa wasimamizi wa uchaguzi huo, hasa wakurugenzi wa halmashauri.

Miongoni mwa vilio ni mawakala kutopewa nakala za viapo vyao na wakurugenzi, kwa ajili ya kuwakilisha vyama vyao katika uchaguzi na kusababisha sintofahamu hasa wanapokwama kuingia kwenye vyumba vya kupigia kura na kuanza usimamizi.

Wakuu hao wa halmashauri pia wamekuwa wakilalamikiwa kwa kutowatangaza wagombea wa vyama hivyo walioshinda, badala yake wanawatangaza wa chama tawala na hivyo kuzusha sintofahamu na malalamiko.

Kutokana na mazingira hayo, jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika zikiwamo za kwenda mahakamani kupinga wakurugenzi hao kusimamia uchaguzi, ili Tume ya Taifa ya Uchaguzi iwe na watumishi wake.

Katika jitihada hizo hivi karibuni Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu iliamuru serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Kesi hiyo ilikuwa inapinga kifungu cha 6(1), 7(1), 7(2) and 7(3) cha Sheria ya Uchaguzi ambavyo vinaruhusu wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi.

Baada ya hukumu hiyo Nipashe inazungumza na wachambuzi wa siasa, wadau wa demokrasia na masuala ya utawala bora na wanasiasa kufahamu kile kilichojiri.



Jaji Jacob Mwambegele, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

Akitoa ya moyoni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anasema ni wakati kwa NEC kuwa na watumishi wa ngazi zote ili kuondoa kasoro ambazo hujitokeza katika uchaguzi.

Ngawaiya, anataja moja ya kasoro hizo kuwa ni tuhuma kwa wakurugenzi kuwazuia mawakala wa vyama kuingia kwenye vyumba vya kupigia kura, kuwanyima nakala za viapo kutokana na kwamba baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi ni makada CCM.

"CEGODETA tunajua kuwa uchaguzi hukumbwa na kasoro nyingi zikiwamo hizo, kutokana na kwamba baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri ni makada wa CCM, hivyo uamuzi wa Mahakama ya Afrika kuzuia wakurugenzi hao ni sahihi," anasema Ngawaiya.

Mwenyekiti wa CEGODETA anasema taasisi hiyo ya utawala bora, inaamini kuwa NEC ikiwa na watumishi wake wa ngazi zote, hakutakuwa na kasoro zisizo za lazima ambazo anadai husababishwa na wakurugenzi hao.

"Wengine husababisha kasoro zisizo za lazima katika uchaguzi kwa ajili ya kulinda vibarua vyao na wengine ni makada, lakini kama tume itakuwa na watumishi wake, unafuu unaweza kuwapo," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema mtindo huo wa kutumia wakurugenzi wa halmashauri, umekuwa ukilalamikiwa kuwa umesababisha wananchi kupata viongozi wanasiowachagua na manung'uniko mengi.

"Sisi taasisi ya utawala bora tunaipongeza mahakama kwa kuliona tatizo hilo na kuamua kuwa wasisimamie uchaguzi, hivyo ingekuwa ni vyema kama uamuzi huo utaheshimiwa," anasema.

**MFUMO UFUMULIWE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, anashauri kuwa kama serikali inataka wakurugenzi hao waendelee kusimamia uchaguzi, mfumo wa kuwapata ufumuliwe.

Dk. Anna anasema wasimamizi wa uchaguzi hawapaswi kuwa watu wanaoegemea upande wowote wa vyama, badala yake wasimamie haki ili demokrasi iweze kushamiri.

"Ninasema hivyo kwa sababu, tulifanya utafiti mwaka 2015 ili kuangalia utendaji wa wakurugenzi na kubaini wengi ni makada wanaoshindwa kura za maoni na kuteuliwa kushika nafasi hiyo," anadai.

Anasema kwa mazingira kama hayo si rahisi mkurugenzi kukubali chama chake kianguke katika uchaguzi na kwamba atafanya kila liwezekanalo kishinde hata kama wapigakura hawamtaki mgombea wake.

"Kwa mazingira kama hayo, ni wazi hakuna demokrasia, hivyo kilichofanywa na mahakama ni kutaka uchaguzi usimamiwe na watu huru, nami ninaunga mkono hilo," anasema Dk. Anna.

Anafafanua kuwa katika hali ya kawaida, si rahisi mkurugenzi ambaye ameteuliwa na mkuu wa nchi akubali chama chake kishindwe na kwamba ili kuwa na demokrasia ya kweli, ni tume kuwa na watumishi wake au kuwa na watu huru wa kusimamia uchaguzi.

**WATANZANIA WAHUSIKE**

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema Mwenyekiti mstaafu wa NEC, Jaji Damian Lubuva, mwaka jana alikaririwa na vyombo vya habari akiishauri serikali kutazama upya utaratibu wa kupatikana kwa watendaji wakuu wa taasisi hiyo ili kutoa fursa kwa Watanzania kuongeza imani na watumishi hao.

"Nakumbuka alisema ili kurejesha imani kwa chombo hicho kinachosimamia uchaguzi, kiundwe chombo kidogo, kitakachoongozwa na Jaji Mkuu na

**INAENDELEA UK. 14**

# Wafuatiliaji watafuta sababu wazungumzaji Kiswahili kuongezeka kufikia milioni 500

**Na Michael Eneza**

AFRIKA ilichukuliwa kama Mnara wa Babeli kwa kukosekana mawasiliano, maana unapovuka mpaka kwenda popote barani humu, unaweza kuwa bubu kama huzungumzi Kiingereza, Kiarabu, Kireno au Kifaransa.

Ni bara linalokosa lugha ya asili ya mawasiliano, badala yake ikitegemea zaidi zile za wakoloni hasa Waingereza na Wafaransa na kukwamisha mawasiliano.

Sasa ni zama mpya, Siku ya Kiswahili Duniani inayofanyika Julai 7, inaanza kusherehekewa maeneo kadhaa, ikiwamo Marekani na hapa nchini, wadau wakianza kuitangaza lugha hiyo inavyoelekea kuiunganisha Afrika.

Ni lugha inayopigiwa chapuo kuwaunganisha wana Afrika Mashariki, Umoja wa Afrika na sasa ndiyo lugha rasmi kwenye masuala ya Shirika la Utamaduni na Elimu la Umoja wa Mataifa (UNESCO).

Hivi karibuni ubalozi wa Marekani katika kusanyiko la kitaaluma unasema matumizi ya Kiswahili nchini humo yameongezeka hasa kuwapo kwa vyuo vikuu vingi ambavyo Kiswahili kinafundishwa, na idadi ya wazungumzaji inavyoongezeka.

Christine Mushi, Katibu wa Baraza la Kiswahili (BAKITA) analiambia kusanyiko hilo la kisomi, kuwa idadi wazungumzaji wa Kiswahili imefikia milioni 500 duniani kote.

Kwa jumla waliojadili tukio hilo walikubalina na takwimu hizo kama uhalisia wenyewe. Si rahisi hata hivyo kuona ni vipi zimepatikana.

Unaweza kusema watu wanaofikia zaidi ya milioni 300 wamekuwa na ukaribu kiasi fulani na Kiswahili kote duniani, sehemu yake kubwa ikiwa ni Afrika Mashariki na hasa Kenya ukiacha Tanzania. Burundi wanazungumza Kiswahili kwa urahisi zaidi kuliko Rwanda au Uganda, wakati mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo takriban kila mtu anaongea Kiswahili.

Siyo rahisi kuchukulia ukanda wa Afrika Mashariki wote kuwa ni wa wazungumzaji wa Kiswahili, vile maeneo hutofautiana ndani ya nchi.

Kinachoshangaza labda ni uelekeo wa kujifunza Kiswahili miongoni mwa wanadiplomasia na washiriki makundi ya kijamii hasa ya vijana wa kujitolea wanaotaka kufanya kazi huku.

Licha ya kuwa uzoefu unaonyesha kuwa mtu akijua lugha kubwa zaidi ya kigeni anaweza kufanya kazi kokote Afrika Mashariki, wengi wanajifunza Kiswahili kama nyenzo ya mawasiliano na wenyeji.

Wafanyakazi wa kampuni za China mara nyingi wanajua lugha yao halafu wamejifunza Kiswahili, bila kutanguliza Kiingereza.

Kitaaluma, hali hiyo inaonyesha kuwa mahusiano ya moja kwa moja ya kijamii au kielimu yanaonyezeka, ambako wageni wanapendelea kuwa na uwezo wa kuzungumza na watu wa kawaida na hata kuchanganyika nao kama wanapewa shughuli za kufanya huku.



Mwalimu Julius Nyerere, mwendelezaji na mtetezi namba moja wa Kiswahili duniani **PICHA: MTANDAO**

Pia aina za shughuli inaelekea ni za kujituma wao wenyewe, kwani wanaopewa majukumu ya kibalozi hawana ulazima wa kufahamu lugha ya mahali wanapokwenda kwa undani. Inatosha kuijua lugha kuu ya kiofisi inayotumika hapo na hapa ni Kiingereza.

Wakati ambao mikutano ya hadhara na hata majadilino bungeni kwa majirani wa Tanzania mara nyingi hufanywa kwa Kiingereza bila kuwa na mashaka baadhi ya wasikilizaji hawatawaelewa kwa wanaotaka kuja Tanzania ni bora wakafahamu Kiswahili.

Huwezi kuwa na uhakika kuwa nusu ya wasikilizaji wanafuatilia vyema kinachosemwa kwa Kiingereza, katika hadhara yoyote nchini, ila kwa kupachika neno la hapa na pale, ni rahisi kueleweka.

Bado vyombo vya habari vina kanuni ya kutafsiri lakini kuna ishara kuwa imepungua, tofauti na miaka michache iliyopita ilivyokuwa.

Wakati nchi za nje zinajifunza Kiswahili kwa wepesi zaidi, hapa nchini kuna mvutano wa kutafsiri hali hiyo, ambao kwa hisia tofauti ulionekana katika hadhara ya hivi karibuni.

Kumsikiliza ofisa wa ngazi ya juu ya ubalozi wa Marekani akiongea Kiswahili kwa ufasaha ilionyesha kuwa ni mojawapo ya mahitaji yake kama mwanadiplomasia, hasa kama nchi yake inamtaka awepo kwa muda mrefu.

Anawasaidia wageni kuelewa nini wengi wa wananchi wanazungumza, au nini kitazamiwe katika nyanja tofauti kijamii.

Kwa mfano ofisa wa ubalozi anayeongea Kiingereza muda wote, anafuatilia masuala ya haki za binadamu na atakuwa na ufinyu wa kile ambacho kinamfikia, kuwa kinapokuwa katika lugha ya kigeni, tayari kimelengwa kwa ajili yake na wafuatiliaji wengine wanaofanana na yeye. Siyo rahisi kujua kama ng'ambo wanazungumza kwa mwelekeo huo au hapana, hivyo kuzishauri serikali za nchi zao kwa kusikiliza vyama vya siasa na AZAKI. Kujua mwananchi wa kawaida anafikiria nini, au wakiwa katika makundi ya jamii wanazungumza nini, huna budi ujue Kiswahili.

Wadau wa matumizi ya Kiswahili katika ngazi zote za elimu wanafarijika na takwimu hiyo ya wazungumzaji milioni 500, na ufasaha wa Ofisa Ubalozi ukionyesha kuwa Kiswahili kinaheshimiwa na hakuna haja ya kuona aibu kutumia Kiswahili katika ngazi zote.

Fikra hiyo ina wadau lukuki ikiwamo BAKITA lakini bado wapo wengi katika jamii na hata serikalini ambao hawajaridhishwa na mwelekeo huo.

Ndiyo lengo la sera mpya ya elimu, kufuta mtihani darasa la saba na kufanya elimu ya sekondari iwe sehemu ya elimu ya lazima, ikitumia Kiswahili.

Endapo Kiswahili kitaachwa sekondari, haitawezekana kukitumia vyuoni na hasa katika wimbi hili la kuajirika wahitimu kwa kujifunza kilimo, useremala na upishi.

Kuna hatari ya mporomoko wa elimu unaoendeshwa na mkakati wa lugha. Rais mstaafu Jakaya Kikwete anaonya juu ya hatari ya kuvuruga ubora wa elimu katika mapitio ya sera ya elimu ambayo baadhi ya wadau wanasema imekamilika na hata Rais Samia Suluhu Hassan aliwahi kugusia jambo hilo, kwa dhamira ya kupongeza.

Wakati akiwa madarakani, Rais Kikwete aliipeleka bungeni hoja hiyo kipindi cha bajeti 2014, ikapitishwa na wabunge wachache waliokuwepo. Haikufuatiliwa tena bunge liliporudi mwisho wa mwaka na mwaka 2016 serikali mpya ikaiacha pembeni.

KINAMAMA WATIANIA 2025

# Waambiwa tafuteni mbinu za kuingia ulingoni kutoka kwa watangulizi wenu




Mwakilishi mstaafu katika Jimbo la Magomeni (CCM), Hafsa Said Khamis, akitoa ushuhuda wa harakati za uongozi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ILI kuongeza ushiriki wa wanawake ndani ya vyombo vya uamuzi, wenye ndoto za kugombea uongozi wameshauriwa kuanza kujifunza na kuchota ujuzi kutoka kwa kinamama wanasiasa wenzao waliowatangulia.

Kushirikiana nao kutawaongezea ujasiri na uthubutu wa kukabiliana na vikwazo kuelekea uchaguzi mkuu 2025, ambao wanawake wengi wanatazamiwa kushiriki.

Ni ushauri wa Mwana Masoud Ali, mwanasiasa mkongwe na mbunge mstaafu wa CUF aliyelitumikia Jimbo la Mtambwe Pemba.

Anakumbusha kuwa ili wenye nia ya kugombea waweze kujua pa kuanzia ili kufanikiwa kiuongozi ni lazima kujifunza kutoka kwa wenzao kuwaelekeza namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili wanapojitokeza kugombea.

Anasema kuwa wanapojitokeza kugombea nafasi za uongozi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kwenye jamii kutokana na mfumo dume uliojengeka hivyo inahitaji utayari na kujiandaa mapema kukabiliana na vikwazo hivyo bila kukata tamaa.

Anataja baadhi ya matatizo yanazowakabili wanawake kuwa ni rushwa, mitazamo hasi ya jamii kuhusu maadili na uwezo wa wanawake kwenye uongozi hivyo ni lazima wanawake wenye nia ya kugombea kujitayarisha mapema kukabiliana na mazingira ya vikwazo hivyo.

"Unapokuwa kiongozi, kwanza unatakiwa kuwa mvumilivu na jasiri, kwasababu sio wote watakupenda na kukuunga mkono wapo watakaokubeza na kukuzarau," anasema.

Anatoa rai kwa wenye nia kugombea kwenye uchaguzi mkuu 2025 washirikiane na wanasiasa wanawake waliowatangulia itawasaidia kuwaongezea ujasiri na kuwapa mbinu zitakazowawesha kushinda katika uchaguzi huo bila kukubali kutumiwa kwa kuwanufaisha wengine.

Lela Nassor Khamis, mbunge mstaafu Jimbo la Chonga (CCM), anataja heshima na kujithamini kuwa ni nguzo muhimu kwa mwanamke anapohitaji kugombea uongozi ili kutotoa nafasi kwa jamii kuchukulia kasoro hizo kama sababu zya kukosa imani na uwezo wa wanawake kwenye uongozi.

"Mwanamke ukiwa kiongozi lazima ujiheshimu, unatakiwa uthamini uanamke wako, ukijithamini hakuna mtu yeyote ataweza kukuvunjia heshima pale unapohitaji kuwa kiongozi.

Na hayo yote unatakiwa kuanza kuyaonyesha kwa jamii yako kuanzia sasa na sio kusubiri mpaka uchaguzi unapofika.

Mwanasiasa mkongwe huyo anapongeza juhudi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA Zanzibar) kwa kuona umuhimu wa kuanza kuwajengea uwezo wanawake wenye malengo ya kugombea uongozi uchaguzi mkuu ambapo itasaidia kuwatayarisha kujitambua na kujua wajibu wao kama viongozi kabla ya kugombea.

"Nimefurahi kuona kwamba TAMWA Zanzibar inatoa mafunzo na kuwapika ili wawe viongozi, nina imani mafunzo haya yatatusaidia kupata viongozi bora kwa sababu huwezi kufikia uongozi bora bila mafunzo ili kujua unfanya nini, lakini kuhimili na utayari wa kukabiliana na vikwazo wakati wa kampeni," anaeleza.

Stara Khamis, mwanasiasa mwenye nia ya kugombea anasema fursa wanayopata kutoka TAMWA ya kuelimishwa namna ya kujiandaa kugombea uongozi kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025 imemwezesha kuwafikia wanawake 47 na kuwahamasisha wawe tayari kugombea nafasi mbalimbali za kuongeza ushiriki katika vyombo vya maamuzi.

Alieleza: "Tangu nianze kupata mafunzo na kujengewa uwezo wa kugombea, nimeamua kutumia elimu hiyo niliyopata kuwahamasisha wanawake vijana wanawake. Nashukuru nimewahamasisha vijana 45 wa wadi yangu ya Madungu waondoe hofu kugombea uongozi kwasababu wanawake wengi wanakuwa na hofu kuingia katika uongozi hasa vijana kutokana na kukosa misingi na elimu sahihi ya uongozi."

Anaongeza, "TAMWA inatupa mwelekeo na njia ya kufikia malengo yetu katika uongozi. Ni jukumu letu tusiangushe juhudi hizi tuingie katika uongozi ili tufikie malengo ya usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya maamuzi."

> "Mwanamke ukiwa kiongozi lazima ujiheshimu, unatakiwa uthamini uanamke wako, ukijithamini hakuna mtu yeyote ataweza kukuvunjia heshima pale unapohitaji kuwa kiongozi.

Mratibu wa TAMWA Ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, anawataka wanasiasa wanawake kutumia fursa ya kukutanishwa na wanasiasa wakongwe kujifunza na kupata uzoefu utakaowasaidia kujenga ujasiri wa kukabiliana na vikwazo wakati wa kugombea.

Anafahamisha kwamba TAMWA kupitia mradi wa SWIL kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway imeandaa jukwaa la kuwaweka pamoja wanawake wanasiasa wapate fursa ya kujengeana uwezo na kuongeza mashirikiano kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025.

Balozi wa Norway, Elisabeth Jacobsen, anasema upo umuhimu mkubwa wa kuendelea kuwaunga mkono wanawake ili kushika nafasi za uongozi pamoja na kuingia katika vyombo vya uamuzi vya kutunga sheria.

Anasema Norway ni miongoni nchi marafiki wakubwa wa Tanzania na uhusiano wake upo tangu miaka 60 iliopita ukijikita katika sekta mbalimbali za kiuchumi na masuala ya usawa wa kijinsia.

Anasema wataendelea kufungua milango kwa asasi za kiraia kuona kwamba zinayafikia malengo yake waliojiwekea ikiwemo kufikisha wanawake kwenye uongozi na kuwainua kiuchumi.

Anasema wanawake wanayo nafasi kubwa ya kushika nafasi za juu za uongozi kama watajengewa uwezo wa uthubutu na kujiamini kwa ajili ya maandalizi ya kushika madaraka ya uongozi.

Aidha, anazitaka asasi za kiraia kuendelea kutoa elimu zaidi kuhusu mbinu za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo matukio ya ubakaji ambao waathirika wake wakubwa ni wanawake na watoto.

Viongozi wa kisiasa wawatoa hofu wanawake, vyama vya siasa vikiwaarifu kuwa milango iko wazi kushiriki katika nafasi za kisiasa na kugombea uongozi majimboni bila vikwazo.

Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya CCM, Khamis Mbeto Khamis, anasema wanawake wameonyesha uwezo mkubwa katika kuwania nafasi za uongozi kwenye ngazi mbalimbali kwa mafanikio kuanzia uwaziri hadi majimboni.

Kwa mfano anasema kwa upande wa CCM kwa muda mrefu imejenga misingi bora na imara ambayo imewawezesha wanawake kufikia dhamira za kisiasa za uongozi.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Salum Mwalimu, anawataka kinamama wajitokeze kuwania nafasi za kisiasa katika majimbo ya uchaguzi na kuacha kulemazwa na viti maalumu.

DK. OMAR ALLY JUMA

# Makamu wa Rais wa kwanza, ndani ya vyama vingi, juhudi, kazi alizoasisi bado zinang'ara

**Na Mwandishi Wetu**

DK. Omar Ali Juma, aliyezaliwa Juni 26, 1941 Chakechake, Pemba, ni mwanasiasa ambaye hatasahaulika.

Anakuwa Makumu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa kwanza baada ya uchaguzi mkuu wa kwanza unaovishirikisha vyama vingi 2015.

Ni mwanamapinduzi aliyekuwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar kuanzia Januari 25, 1988 hadi Oktoba 1995 ni kuanzia hapo hadi alikuwa Makamu wa Tanzania, katika awamu ya tatu iliyoongozwa na Benjamin Mkapa.

Julai 4, 2001, Dk. Omary Ali Juma, alifariki dunia jijini Dar es Salaam na kufunga ukurasa wa kazi nyingi za kisiasa alizozifanya Bara na Visiwani lakini akiwaachia Watanzania urathi (legacy), inayoendelea kuishi hadi sasa.

Msomi huyo anaanzia safari ya kusoma katika katika ya nwaka 1947 na 1960 katika Shule ya Wavulana ya Chakechake na baada ya hapo Sekondari ya Ian Smith leo Haile Selassie.

Alijiunga na Chuo Kikuu cha Moscow, baadaye Chuo Kikuu cha Cairo na huko kote akisema masuala ya tiba ya mifugo na upasuaji wanyama.

Kifo cha Omar kiliwashtua Watanzania na kuwashangaza kikitokea kutokana na mshtuko wa moyo, akifariki kabla ya saa sita usiku Julai 4, 2001.

Kifo cha Dk. Juma kilizidi kustaajabisha kwa sababu siku hiyo alikuwa ameamka mzima akifanya shughuli za kiserikali kwenye makazi yake ya Oyster Bay jijini Dar es Salaam na kisha kwenda kwenye ufunguzi wa Maonyesho ya Sabasaba ndani ya Viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Hata hivyo walikipokea kwa sababu hakuna anayejua siku wala saa ya kufa kwake, wala ya kuzaliwa, hivyo yote ni ya Mungu.



Dk. Omar enzi za uhai wake.
**PICHA: MTANDAO**

Miaka 22 imepita tangu mwanasiasa huyo atwaliwe, lakini mengi yanaendelea kulipamba jina lake na kuenzi kazi yake. Akiwa namba mbili kwenye safu ya viongozi wa serikali, Dk. Omar alifanyakazi kazi ya kumshauri Mkapa kufanya mambo makubwa ambayo ni kama kuingiza mashaua au merikebu ndani ya maji au bahari usiyoifahamu.

Ni kutoka na wakati huo Tanzania kuingia katika mfumo wa vyama vingi ambavyo waliongoza taifa katika mfumo ambao si wao wala Watanzania walifahamu wali kubashiri kuwa itakuwaje na nini hatima ya kuwa na siasa za vyama vingi.

Ndizo zilikuwa zama za kufanya mapinduzi ya kiuchumi na kuweka sawa mwelekeo wa mapinduzi ya kuiondoa sekta ya umma kwenye uzalishaji na kuiimarisha binafsi pia kulikubali na kuligeukia soko huria na utandawazi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika jukumu lake la ushauri kulikuwapo na mambo mengi ukiwamo mkwamo wa kisiasa baina ya CUF na CCM Zanzibar, uliotokea baada ya uchaguzi mkuu wa vyama vingi 1995.

Ndiyo wakati ambao Makamu wa Rais Dk. Omar alifanyakazi kwa bidii na bosi wake Mkapa pamoja na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola, Chief Emeka Anyaoku, kufikia suluhisho la mgogoro huo wa kisiasa na kupata mwafaka.

Itakumbukwa mgogoro wa kisiasa ulitokana na matokeo ya uchaguzi mkuu wa 1995 visiwani Zanzibar, wakati huo CUF ikitangaza kuwa imeshinda na kuporwa ushindi na CC.

Wakati wa uhai wake aliamini kujenga dira mpya ya vyama vingi kuwa ni nguvu ya kuwa na Muungano na Tanzania na Zanzibar imara ambazo zitashikamana na kuachana na mivutano wa kisiasa.

Hata leo Zanzibar, kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa SUK, ambayo Dk. Omar ana mkono wake kwenye kuhakikisha umoja na mshikamano wa taifa.

Kwa kushirikiana na Mkapa wawili hawa walifanya mageuzi makubwa kisiasa na kiuchumi na kuibadilisha Tanzania kiuchumi na kisiasa kwa kuweka masuala makubwa ikiwamo ubinafsishaji wa mashirika yaliyoitwa mizigo na kuanzisha wakala mbalimbali za serikali kuchukua nafasi za baadhi ya taasisi hizo za umma.

Mojawapo ya mashirika makubwa yaliyobinafsishwa ni pamoja na kampuni ya sigara TCC, kiwanda cha bia lakini pia ukawa ujio wa Wakala wa Taifa wa Barabara (TANROADS), kadhalika mamlaka kama ya mapato TRA, usimamizi wa usafirishaji ardhini na nchi kavu SUMATRA sasa LATRA ziliundwa na taasisi nyingi binafsi za fedha ziliruhusiwa kufanyakazi zikiwamo maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.

Licha ya kwamba Makamu wa Rais Dk. Omar pamoja Mkapa wametwaliwa kila mwaka Julai Watanzania wanawakumbuka na kuwaenzi na kutokana na kazi kubwa ya maendeleo waliyoianzisha ili kubadilisha taifa lao ili kufikia hatima ya maisha bora kwa kila mmoja.

# Wadau wanavyoshangilia kuengua wakurugenzi kusimamia uchaguzi

**INATOKA UK. 11**

wajumbe wengine, ambao watakuwa wanawafanyia usaili watumishi wanaoomba kuongoza NEC," anasema Magdalena.

Katika ufafanuzi wake, anasema Jaji Lubuva anashauri chombo hicho kuwa kiwe ndicho kiwashindanishe kwa vigezo na sifa zinazotakiwa, kabla na kuwasilisha majina watakaopelekwa Ikulu kuteuliwa.

"Ninaunga mkono uamuzi wa mahakama kwani hicho ndicho kilio cha muda mrefu cha wapinzani. Sasa baada ya hukumu hiyo, ni vyema ushauri uliotolewa na Jaji Lubuva uzingatiwe," anasema.

Anasema ushauri huo wa Jaji Lubuva ambayo ni maoni yake kwenye kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa na hukumu ya mahakama hiyo, vimetolewa kwa wakati mwafaka, na kwamba kinachosubiriwa ni utekelezaji.

Itakumbukwa kuwa Bob Wangwe na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), walifungua kesi Na 011/2020 dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Kesi hiyo ilikuwa inapinga kifungu cha 6(1), 7(1), 7(2) na 7(3) cha Sheria ya Uchaguzi ambavyo vinaruhusu wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi nchini.

Mahakama hiyo ikatoa uamuzi kwamba vifungu vinakiuka ibara ya 13(1) ya Mkataba wa Afrika unaotoa haki ya kila mtu kushiriki katika uongozi wa nchi kwa kuchaguliwa au kupitia wawakilishi kwa mujibu wa sheria.

Uamuzi huo wa mahakama, unaelezwa pia na Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, aliyefungua kesi hiyo na LHRC kwamba ni hatua nzuri ambayo ni mwelekeo wa kufikia demokrasia ya kweli.

Kilichofanyika si haba, ni mwendelezo wa kutafuta demokrasia, kwani haba na haba hujaza kibaba, hivyo kila sehemu ambayo tutaona kuna upungufu tutaendelea kuifanyia kazi," anasema Wangwe.





## Mbunge ahimiza wanawake kutunza chakula

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani, amewaasa wakulima wanawake kutunza chakula baada ya mavuno ili kujiepusha kukumbwa na ukosefu wa chakula.

Kamani ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifunga Mradi wa Kuchechemua Uwekezaji katika Kilimo (SUPIA II), unaotekelezwa na Shirika la ActionAid Tanzania.

Alisema familia ikikosa chakula aibu humkuta mama huku akiwataka kupata elimu ya utunzaji wa chakula.

"Katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi tumeahidi tutaendelea kuhakikisha tunapunguza upotevu wa chakula baada ya mavuno, kaya ikipata njaa anayeaibika ni mama, tunaweza kuwa tunafanya vizuri shambani, tunavuna vizuri lakini tusipopata elimu tunaweza kujikuta tunapoteza chakula kwa wingi sana," alisema.

Aliwataka wakulima hao wanatakiwa kuwa kinara katika kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi ili kukomboa mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti.

Naye Katibu Mkuu wa Jukwaa la Wakulima Wanawake Tanzania, Anastazia Madeje, alisema ujio wa mradi huo umewabadilisha wanawake na umewawezesha kushiriki kwa ufanisi katika ngazi mbalimbali za maamuzi ili kufuatilia haki zao.

Mkulima kutoka Singida, Fredina Makeleja alisema pamoja na mafanikio waliyoyapata katika mradi huo bado wameitaka serikali kuendelea kuwatumia katika uchambuzi wa bajeti ili kujua bajeti inayotengwa inakidhi mahitaji kwa wakulima.

"Serikali itushirikishe katika kuandaa mipango ya kukuza kilimo na kuyashirikisha majukwaa ya wakulima kuendeleza mradi ili kuleta matokeo chanya," alisema Makeleja.

Mkurugenzi wa Shirika la Actionaid Tanzania, Bavon Christopher, alisema licha ya muda huo kuisha lakini wakulima wanapaswa kutumia maarifa waliyoyapata ipasavyo.

# Dk. Shoo aitaka jamii kuacha mila na desturi kandamizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, ameitaka jamii kuachana na mila na desturi kandamizi hususani ndoa za utotoni kwa kuwa zinasababisha kutengeneza kizazi kisicho salama.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa mradi wa 'Hapana marefu yasiyo na mwisho' uliopo chini ya kanisa hilo, Askofu Shoo alisema vitendo hivyo vinaathiri kwa kiasi kikubwa watoto na kwamba ni jukumu la jamii kuondokana na mila hizo.

"Sisi ni Tanzania kwanza kama kuna jambo linamhusu mtoto wa kitanzania ni la kwetu sote bila kujali tofauti ya dini zetu," alisema.

Aliongeza: "Kazi yetu kuu ya kueneza injili, lakini pia tunatoa huduma za kijamii kwa sababu hata Yesu Kristo mwenyewe alizifanya, kwani siyo sawa kuitwa kanisa kama hatuwezi kumuhudumia mwanadamu kiroho kimwili na kiakili," alisema.

Dk. Shoo alisema wanatamani kutokomeza ndoa za utotoni na kuleta mabadiliko ya kisheria.

"Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, tunaona inahitaji mabadiliko, mtoto wa kike wa miaka 14, 16 au 17 hawa bado ni watoto, hivyo tutashirikiana na serikali kuona mabadiliko yanatokea," alisema.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii nchini, Dk. Nandera Mhando, alisema takwimu za utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria kupitia viashiria vya mwaka 2022 zinaonesha wasichana 418 hawakumaliza elimu ya msingi kwa sababu ya mimba.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya utafiti huo mwaka 2015/16 asilimia 27 ya wasichana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 19 wamepata ujauzito kwa mikoa ya katavi (45%), Tabora (43%), Dodoma (39%), Morogoro (39%) na Mara (37%).

Hata hivyo alisema mradi huo utaongeza wigo wa afua za kupambana na ndoa za utotoni hivyo alitoa rai kwa viongozi wa dini wakati mchakato wa kuzifanyia mabadiliko sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ukiendelea, watoe maoni yao ili yajumuishwe kabla ya kupelekwa bungeni.

"Mimba za utotoni bado ni tatizo kubwa na kikwazo kikubwa kwa wasichana kukamilisha mzunguko wao wa elimu hapa nchini na ndoto zao. Mimba za utotoni licha ya kuzorotesha masomo ya mtoto wa kike, pia zina madhara ya kiafya yaani husababisha ongezeko la vifo vya mama na mtoto hapa nchini," alisema.

Mratibu wa Mradi, Patricia Mwaikenda alisema unategemea kuwafikia watoto wa kike 2400 kwenye vijiji 24 na maeneo lengwa ni Zanzibar, Tabora, Morogoro, Mwanza na Dodoma na utakuwa wa miaka mitatu na utatumia Sh.bilioni 2.5.



Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kanali Regina Matina (katikati), akishiriki kufanya usafi wa mazingira katika eneo la Kituo cha Afya cha Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Elimu yasaidia kupunguza matukio ya ukeketaji Singida

**Na Renatha Msungu,** SINGIDA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali la Woman Wake Up (Wowap), limesema kampeni za utoaji elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji zinazofanyika kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye minada zimechangia kupunguza vitendo hivyo mkoani Singida.

Akizungumza juzi na wananchi kwenye mnada wa Kijiji cha Merya wilayani Singida, Mratibu wa shirika hilo, Nasra Suleiman alisema kampeni hizo zinafanyika kupitia mradi wa kupinga vitendo vya ukeketaji unaofadhiliwa na Shirika la Woman Actions Against FGM (WAAF) nchini Japan na unatekelezwa kwenye mikoa ya Dodoma na Singida.

"Tumekuwa tukitoa elimu kwenye minada kwa sababu inakusanya watu wengi, tumefika na kutoa elimu hapa, mwitikio ni mkubwa na wengi waliuliza maswali hasa kuhusiana na suala la adhabu," alisema Suleiman.

Alisema mpango wa taifa wa utekelezaji wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa mwaka 2017- 2018, 2021-2022 umeeleza kwa ufasaha kwamba ukeketaji ni mila inayoathiri wanawake na watoto, hivyo haipaswi kufanywa.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoani humo, Shukrani Mbago, alisema wanaendelea kutoa elimu ili wananchi waachane na mila ya ukeketaji.

Alisema wao kwa kushirikiana na WOWAP wametoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ili waache vitendo vya ukeketaji kwa jamii.

Mmoja wakazi wa kijiji hicho, Asha Senge, alisema hivi sasa jamii imeelimika kupitia mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali baada ya kupata kupata elimu juu ya madhara wanayopata wasichana baada ya kufanyiwa ukeketaji.

Alisema jitihada za serikali kwa kushirikiana na taasisi hizo imekuwa chachu kubwa kwa jamii kuelimika hususani mangariba ambao wanahusika kwa kufanya vitendo hivyo katika vijiji mbalimbali hapa nchini.

Alisema: "Tunaishukuru sana serikali kwa ushirikiano wanaotoa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kutekeleza miradi balimbali ya utoaji elimu ya kupinga masuala ya ukeketaji".





# Lumbesa yawatesa wakulima wa viazi mviringo

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAKULIMA wa viazi mviringo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kutokomeza vipimo vinavyozidi ujazo maarufu kwa jina la lumbesa wakidai kuwa vinawaumiza.

Wakulima hao wanadai kuwa liche ya serikali kupiga marufuku vipimo hivyo lakini wafanyabiashara wanaendelea kuvitumia huku halmashauri ikitumia tatizo hilo kama chanzo cha mapato kwa kuwatoza faini wafanyabiashara.

Wanadai kuwa kitendo cha halmashauri kuwatoza faini wafanyabiashara hao, kinawaumiza zaidi wakulima kutokana na wafanyabiashara kupunguza bei ya kununulia zao hilo ili kufidia faini wanazotozwa na serikali.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wakulima wa Kata ya Ndato ambayo ni miongoni mwa kata zinazoongoza kwa uzalishaji wa viazi mviringo katika Halmashauri ya Rungwe walisema tatizo hilo limekuwa sugu.

Mmoja wa wakulima hao, Asheri Ngomano alisema wanunuzi wa viazi wanagoma kununua viazi kwa wakulima wanaogomea rumbesa hali inayosababisha wakulima kulazimika kuwakubalia ili kufidia ghrama za uzalishaji.

Alisema wanunuzi hao wanapofika kwenye mageti ya halmashauri wanatozwa faini ya Sh. 300,000 na kuruhusiwa kuendelea na safari jambo ambalo linasababisha tatizo hilo kuendelea kuwapo.

"Mnunuzi wa viazi anashona lumbesa ambayo serikali imepiga marufuku na akifika getini anatozwa faini kisha anaruhusiwa kuendelea na safari, sasa hiki kinachofanyika ni sawa na mtu akamatwe na bangi halafu atozwe faini na kuachiwa aende na bangi yake," alisema Ngomano.

Alisema faini wanazotozwa wanunuzi wa viazi zinalipwa na wakulima kutokana na wanunuzi hao kushusha bei ili kufidia faini wanazotozwa na halmashauri.

Naye Farda Haruna alisema tatizo lingine linalowakabili wakulima wa zao hilo ni uuzaji wa viazi kwa kupitia madalali ambao ndio wanaoshusha bei na kuwalazimisha kushona lumbesa.

Alisema kutokana na tatizo hilo sasa hivi viazi vimeshuka kutoka Sh. 80,000 waliyokuwa wanauza kwa mfuko mmoja mpaka Sh. 30,000 na kwamba madalali wanagoma kununua viazi bila kushona lumbesa.

Alisema wanapohoji sababu ya kushuka kwa bei hiyo wanaambiwa kuwa wanafidia faini ambazo wanatozwa na maofisa wa serikali kwenye mageti.

"Sisi tunashindwa kuelewa kwamba hizi faini anatakiwa kutozwa mfanyabiashara ama sisi wakulima? Maana madalali wanatukata sisi fedha wanazotozwa kama faini," alihoji Farda.

Sebastian Ngairo alisema tatizo hilo linasababisha baadhi ya wakulima kushindwa kurejesha mikopo wanayochukua kwenye taasisi za kifedha kwa ajili ya uendeshaji wa kilimo hicho.

Alisema kutokana na unyonyaji huo unaofanywa na wanunuzi hata kiwango cha mavuno kimepungua kwa maelezo kuwa shamba ambalo mkulima anatakiwa kuvuna magunia 100 huwa yanashuka mpaka 70 na hivyo kuibiwa magunia 30.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Unyamwanga kilichopo Kata ya Isongole wilayani humo, Daniel Msisyana, alikiri kuendelea kwa ujazo wa lumbesa huku akidai kuwa chanzo ni ushindani wa soko kwa wafanyabiashara.

Alisema tatizo hilo siyo kwa Rungwe pekee bali ni nchi nzima na kwamba wakikataza katika eneo hilo wateja watakimbilia kwenda kununua kwenye maeneo mengine ambayo wakulima wanakubali.

Akizungumzia malalamiko hayo kwa njia ya simu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau alikiri kuendelea kuwapo kwa tatizo hilo na kwamba faini wanazowatoza wafanyabiashara ni utekelezaji wa sheria ndogo za halmashauri hiyo.

Alisema ili kukomesha biashara hiyo kunahitajika ushirikiano baina ya serikali, wakulima na wadau wengine wa kilimo na kwamba tofauti na hivyo tatizo haliwezi kuisha kirahisi.

Mwaka jana viongozi wakuu wa serikali hasa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, walipiga marufuku ujazo huo wa lumbesa na kuagiza viongozi wa serikali katika mikoa mbalimbali kusimamia.



Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi (kulia), akikabidhiwa ofisi na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Wakili Triphonia Kisiga, juzi. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (wa pili kushoto) na Meya wa Jiji hilo, Sheikh Dor-Mohamed Issa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watumishi h/shauri watakiwa kuzingatia sheria, kanuni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATUMISHI wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya wametakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili wananchi wapate huduma wanazostahili na kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Nchimbi alitoa rai hiyo juzi alipokuwa anakabidhiwa ofisi na aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Wakili Triphonia Kisiga.

Alisema kila mtumishi anatakiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo huku akisisitiza ushirikiano baina yao katika kuwahudumia wananchi kama sheria zinavyowataka.

Alisema katika utumishi wake ndani ya Jiji hilo atahakikisha anashirikiana na watumishi wote kuhakikisha maendeleo yanayotarajiwa na serikali yanafikiwa na hakuna migogoro inayotokea. Aliwataka watumishi ambao walikuwa wavivu kwa miaka ya nyuma kubadilika ili kuendana na kasi anayoitaka yeye huku akisisitiza kuwa hatamwonea mtu yeyote bali atahakikisha anatenda haki.

"Mimi naamini kwamba kila mtumishi anakuwa na nafasi ya kubadilika na kuanza upya, kuna watu huwa wanakuwa wazembe wakati anapokuwapo kiongozi fulani na kubadilika baada ya kiongozi mpya kuingia, kwahiyo naamini wale ambao mlikuwa mnazembea mtabadilika," alisema Nchimbi.

Alisema katika kipindi chote atakachokuwa Mkurugenzi wa Jiji hilo atahakikisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia maelekezo halali ya serikali.

Akikabidhi ofisi kwa Nchimbi, aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi, Wakili Triphonia ambaye ni mtumishi katika idara ya sheria wa Jiji hilo alisema ataendelea kushirikiana na kiongozi huyo katika mambo yote ya maendeleo.

Alisema mpaka sasa Jiji hilo linaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo akamwomba kuendelea kuisimamia kwa ukaribu ili ikamilike.

Meya wa Jiji hilo, Sheikh DorMohamed Issa alimpongeza Nchimbi kwa kuaminiwa na Rais Samia Suluhu Hassan na hivyo akamshauri kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha imani aliyopewa inakuwa na matokeo chanya.

Aliwataka wakuu wa idara za halmashauri hiyo kumpa ushirikiano kiongozi huyo ili atimize malengo ya serikali ambayo ametumwa kuyatekeleza. Alisema Baraza la Madiwani la Jiji hilo wataendelea kushirikiana naye kama ambavyo walifanya kwa wakurugenzi wengine ili kuwahudumia wananchi vile inavyostahili.

"Umri wako bado ni kijana na una uwezo wa kukimbizana katika kuwaletea wananchi maendeleo, sisi tuna imani na wewe kwa hiyo tunaamini tutashirikiana vizuri katika kulifanya Jiji letu kuwa la kisasa," alisema DorMohamed.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alimpongeza Kisiga kwa utendaji kazi aliokuwa nao katika kipindi chote alichokaimu nafasi hiyo.

Alimshauri Nchimbi kuendeleza mambo yote mazuri yaliyokuwa tayari yameanzishwa kwa nia ya kuwaletea wananchi maendeleo ya haraka.

Jiji la Mbeya ni miongoni mwa halmashauri ambazo wakurugenzi wamekuwa wakidumu kwa muda mrefu na kuondolewa kutokana na sababu mbalimbali.

## Wakazi Mbeya waeleza fursa kiuchumi ujenzi wa barabara 4

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI jijini Mbeya wamesema ujenzi wa barabara ya njia nne katikati ya Jiji hilo utasaidia kuongeza fursa za kiuchumi pamoja na kuondoa msongamano wa magari ambao umekuwa ukichelewesha baadhi ya shughuli.

Waliyasema hayo jana walipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi huo ambao unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu ambapo walisema utasaidia pia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Mmoja wa wananchi hao, John Mwakabungu alisema kwa muda mrefu kumekuwa na msongamano wa magari katikati ya Jiji na kusababisha baadhi ya shughuli kuchelewa kutekelezwa.

Alisema kumekuwa kukiwa na msongamano mkubwa asubuhi na jioni kutokana na mwingiliano kati ya magari makubwa na madogo pamoja na barabara kuwa nyembamba.

"Tumeona tayari kambi ya mkandarasi imeanza kujenga kule Iwambi, sasa tunaamini kuwa siyo siasa tena, ikikamilika watu watakuwa wanawahi kwenye biashara zao na hata wafanyakazi wa umma watakuwa wanawahi kazini," alisema Mwakabungu.

Rehema Joseph alisema wamepata maelezo kuwa barabara hiyo itakuwa na vivuko vya juu vya watembea kwa miguu na hivyo wanaamini kuwa ajali za watu kugongwa na magari zitapungua. Alisema vilevile serikali imeeleza kuwa zitawekwa taa kwenye maeneo yote ya katikati ya mji jambo ambalo litasaidia kustawi kwa biashara za wananchi.

"Tunamshukuru Rais kwa mradi huu na tunaamini utakamilika kwa wakati na tutaanza kunufaika mapema, tumekuwa tukihangaika kwa muda mrefu," alisema Rehema.

Aliiomba serikali ikikamilisha mradi huo ianze mapema utekelezaji wa mradi wa njia ya mchepuko kwa ajili ya malori ili kuondoa kabisa ajali ambazo zimekuwa zikisababishwa na malori.



## ZSSF yaanza kuhakiki wanachama Zanzibar, Bara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), umeanza zoezi la uhakiki wa wanachama kwa mikoa yote ya Zanzibar na waliopo Tanzania Bara na wanatarajia kuhakiki wastaafu 11,000.

Hayo yamesemwa na Kaimu Meneja wa ZSSF, Zainab Rajab Mbaraka, wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema zoezi hilo litawagusa wastaafu wote ambao wanapokea pensheni kupitia ZSSF, ambalo litamalizika Julai 9, mwaka huu.

Alisema ZSSF imejiandaa kufanya mengi ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za bei nafuu kwa wanachama wa mfuko huo na wastaafu wingine.

Alisema mipango hiyo haiwalengi waliostaafu kipindi hiki tu bali umelenga mpaka wale waliofanya hivyo miaka ya nyuma.

Kaimu Mkuu Kitengo cha Mafao, Mussa Yussuf Mussa, alisema itahakikisha inaweka mipango madhubuti ili kila mstaafu ahakikiwe akiwa nyumbani kwake.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wastaafu Abdulkhakim Mzee na Said Abdurahman walisema wanafarajika kuona ZSSF inafanya uhakiki huo kila baada ya miezi sita kwa lengo la kuwahakikishia usalama wa upatikanaji wa pensheni zao ambazo hutolewa kila mwezi.

Waliomba ZSSF kuwaongeza pensheni kwa sababu wao ndiyo waanzilishi wa mfuko huo kama ilivyozingatia katika nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi wa zamani.

**Alisema mipango hiyo haiwalengi waliostaafu kipindi hiki tu bali umelenga mpaka wale waliofanya hivyo miaka ya nyuma.**

# Makamu wa Rais ahimiza matumizi lugha ya Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema ipo haja ya kuzingatia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili hasa katika vyombo vya habari.

Aliyasema hayo jana wakati akifunguwa kongamano lililowakutanisha wahariri wa habari kuelekea maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani.

Makamu huyo aliwataka wahariri wa habari kuchukua nafasi ya kulinda lugha ya Kiswahili ili kuhakikisha hakuna upotoshaji unaofanywa, ambao utaathiri maendeleo ya lugha hiyo kwa kizazi kijacho.

Alisema ni wakati wa kuweka mikakati kuona lugha ya Kiswahili inatumika vizuri na kuepusha matukio ya uharibifu wake unaotokana na upotoshaji wa makusudi.

Alisema matumizi sahihi na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa yatafunguwa nafasi na fursa kwa vijana mbalimbali kujiajiri katika lugha hiyo nje ya nchi.

Aidha, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) pamoja na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) kuona utafiti zaidi unafanyika katika kukuza lugha ya Kiswahili.

Alisema utafiti huo ni muhimu kwa ajili ya kukiendeleza Kiswahili na kuwa miongoni mwa lugha maarufu inayotumiwa na watu wingi duniani kote.

"Tayari jumla ya vyombo vya habari vya utangazaji redio 38 duniani zinarusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili, hivyo ni vyema waandishi wa habari kuitumia fursa hiyo," alisema.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema wakati umefika kwa vyombo vya habari kukitumia Kiswahili kama ni bidhaa itakayoleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi ikiwamo ajira.

Alisema matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili yatasaidia kupatikana kwa ajira kupitia vyombo mbalimbali vya habari vya nje ya nchi pamoja na kufanya kazi katika taasisi za elimu ya juu.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Khamis Mwinyuma, aliwataka wahariri wa habari kukipa hadhi na nafasi lugha ya Kiswahili ambayo ikipata umaarufu siku hadi siku.

Alisema zipo fursa nyingi za lugha ya Kiswahili katika ngazi ya kimataifa kwa sababu wageni wengi wamekuwa na hamu ya kujifunza lugha hiyo katika kiwango cha kimataifa zaidi.

Akiwasilisha mada isemayo nafasi ya wahariri wakuu katika kusimamia matumizi sanifu katika vyombo vya habari na kulinganisha na vyombo vya habari vya nje, Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Charles Hilary, alisema wahariri wanapaswa kufuatilia na kusimamia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili.

Alisema baadhi ya vyombo vya habari watangazaji wake wengi wanachanganya lugha ya Kiswahili pamoja na Kiingereza na hivyo kuwapo kwa upotoshaji mkubwa.

Akizungumza katika kongamano hilo Katibu Mkuu wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Consalate Mushi, alivitaka vyombo vya habari kuchukua juhudi za kusambaza Kiswahili ili kuwa miongoni mwa lugha bora duniani.



Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde (katikati), akizungumza alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji na miundombinu yake katika kata za Ndungu, Miamba na Kihurio wilayani Same mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaipa zigo SUZA kutangaza Kiswahili kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imekitaka Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), kuendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali ili kupata nguvu katika kutangaza lugha ya Kiswahili nje ya mipaka ya Tanzania.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la shamrashamra ya Siku ya Kiswahili Duniani yaliyofanyika katika chuo hicho Kampasi ya Maruhubi.

Alisema SUZA ni kitovu cha Kiswahili Afrika ya Mashariki, hivyo ushirikiano huo ndio nguzo muhimu itakayoleta tija na sio katika masuala ya kitaaluma bali katika ukuzaji na maendeleo ya Kiswahili kwa ajili ya maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Aidha, alisema kuwa hatua hiyo pia itasaidia kufikia lengo la kuimarisha ustawi wa jamii za wazungumzaji na watumiaji wa lugha ya Kiswahili popote inapotumika.

Waziri Pembe alisema Kiswahili ni lugha ya taifa katika nchi za Tanzania, DRC, Uganda, na Kenya na mojawapo ya lugha rasmi katika shughuli za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Umoja wa Afrika.

Alisema baadhi ya nchi za Afrika zinafundisha au zimeazimia kuanza kufundisha lugha ya Kiswahili katika mifumo yao rasmi ya elimu.

Naye Mkuu wa Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni kutoka SUZA, Dk. Kijakazi Omar Makame, alisema maadhimisho ya Siku ya Kiswahili yanafuatia uamuzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuiteua Julai 7 kuwa siku rasmi ya Kiswahili duniani.

Alisema lugha ya Kiswahili inaendelea kukua na kuwa ni bidhaa muhimu ya mawasiliano kimataifa na kuiomba serikali kutilia nguvu matumizi ya lugha hiyo katika nyanja za kielimu, uchumi, siasa na kijamii.

Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Mohammed Makame Haji, alisema chuo hicho ni miongoni mwa vyuo vikuu ambavyo vipo mstari wa mbele katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini.

Alisema katika kuthamini mchango huo wanapata nguvu na kuendeleza wataalamu wao ili kufikia malengo ya serikali ya kukifanya Kiswahili kuwa ndiyo lugha kuu duniani ambayo inatumika katika sekta zote.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 674 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**MIRIAM EDWIN SICHINGA**
**And**
**In the matter of Application for letters of administration**
**by AISEA IBRAHIM MBOJA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 2 day of 8....2023

**Dated at DAR ES SALAAM this 26 day of 06....2023**

Senior Resident Magistrate

## TANGAZO KUPOTELEWA NA HATI ZA VIWANJA

**JOYCE MOURICE MUGINI** ambaye ni msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Mourice Joseph Mugini.

Anatangaza kupotelewa na hati za viwanja, Kiwanja namba 39 Kitalu"34"Mwanza Road chenye hati namba 4141 LO No 85348 katika Manispaa ya Shinyanga.

Kiwanja kingine namba 9 Kitalu "ZZ" Ibinzamata chenye hati namba 17350 LR Mwanza Na LO No 182653 katika Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Joyce Mugini kwa simu namba 0754-826932.

**Taarifa ya Polisi/SHI/SHI/RB/224329/2023.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS FOR FILING WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(Order V Rule 1(b) CPC)**
**IN THE DISTRICT COURT OF NANYUMBU**
**AT NANYUMBU**
**CIVIL CASE No. 1 of 2023**
**FADHILI CHIKAWE ............................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**JUMA BROWN MWAMLENGA..................DEFENDANT**

**TO:-**
**JUMA BROWN MWAMLENGA**
**OF DAR ES SALAAM**

**WHEREAS** the above named plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim, the particulars of which are set out in the annexed copy of the plaint.

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one days of service of this notice upon you. If there are more than one plaintiffs additional copies of your Written Statement of Defence must be filed sufficient for service on each of the plaintiffs. If there are more than one defendants and the defence is not joint defence, there must be filed sufficient copies for service on each of the other defendants.

**TAKE NOTICE** that the case also has been fixed for mention on the 10 day of JULAI, 2023 at 08:00 am in the forenoon.

**AND TAKE FURTHER NOTICE** that if you default in filing of the Written Statement of defence within the time specified the Court may pronounce judgment against you

**GIVEN UNDER MY HAND AND SEAL OF THE COURT** this 27 day of JUNE 2023

RESIDENT MAGISTRATE IN CHARGE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED** inatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 506 DAX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:
**9910837249433**

## KUPOTEA KWA VYETI



**DOROTHY THOMAS SAMKYI** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha sita chenye index namba S1187/0551 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. MARY GORETTI SECONDARY SCHOOL mwaka 2013.** Na cheti cha shahada ya kwanza kilichotolewa mwaka 2016 na chuo cha **TUMAINI UNIVERSITY DAR ES SALAAM COLLEGE,** cha Bachelor of Business Administration- Marketing and Management, chenye registration namba **TU/DARCO/BBA/013/076.**

Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa vituo vyovyote vya polisi.

**POLISI TAARIFA: WMB/RB/1635/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BWANA TULAONA WILLIAM HAULE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T503 ALS AINA YA FUSO YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KATIKA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARBU NAE JALDA NAMBA IRI/IRI/RB/225512/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA ILEMELA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA TALAKA NA. 121/2022**
**ANNASTAZIA MARWA WANGWE................MDAI MUHUKUMIWA**
**DHIDI YA**
**KENNEDY MWITA GIMUGE................MDAIWA MUHUKUMIWA**

**AMRI YA KUUZA MALI KUTIMIZA HUKUMU**
**(KANUNI YA 72, 73 & 78 YA KANUNI ZA UTARATIBU WA MADAI KATIKA MAHAKAMA ZA MWANZO)**

**KWA; NYADHI INVESTMENT CO.LTD,**
**DALALI WA MAHAKAMA**
**K.K. HAKIMU MKAZI MFAWIDHI,**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA,**
**S.L.P 155 MWANZA.**

KWA HATI HII NAKUAMURU KUUZA KATIKA MNADA WA HADHARA BAADA YA KUTANGAZA KWA MUDA WA SIKU 14 KWA KUBANDIKA KATIKA MBAO ZA MATANGAZO NA NYUMBA YA MDENI MHUKUMIWA IKIELEZA WAKATI WAKATI NA MAHALA PATAKAPOFANYWA MNADA HUU NA MALI ITAKAYOUZWA, NA BAADA YA KUTANGAZWA MALI AMBAYO NI NYUMBA NA. 09 ILIYOPO TANKI LA MAJI NYASAKA (W) ILEMELA MKOA WA MWANZA ILIYOKAMATWA KWA HATI YA KUKAMATIA MALI ILIYOTOLEWA NA MAHAKAMA HII JUMATANO YA TAREHE 28/03/2023 KWA KUTIMIZA HUKUMU YA WADAIWA WALIOTAJWA HAPO JUU, AU MALI ITAKAYOKAMILISHA KIASI CHA SHILINGI 17,000,000/=TZS

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**ILEMELA**
**MWANZA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

GERRY NGOLO LIHEMULA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA TOYOTA HIECE YENYE NAMBA ZA USAJILI T.325 AJP.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/225801

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 15/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ISMAIL MOHAMED KISWANYA wa MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA YUSUPH ISMAIL KISWANYA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **17** Mwezi **07** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 06 mwaka 2023

*OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Majaliwa awapa jukumu ma-DAS kukabili ushoga

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Makatibu Tawala wa Wilaya kusimamia mambo 10, ikiwamo kuzifuatilia taasisi zisizo za serikali zinazojihusisha na vitendo vya ushoga.

Majaliwa pia amekemea migogoro kati yao na wakuu wa wilaya, mihemko na mienendo isiyofaa na kutaka wazingatie miiko na maadili ya viongozi wa umma.

Majaliwa alielekeza hayo jana jijini hapa alipofungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi hao walioteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Alisema kwa sasa taifa lina ajenda ya kupambana na mmomonyoko wa maadili na kuna taasisi katika maeneo yao kupitia ufadhili wanaopata wana kipengele kinawataka waeneze vitendo hivyo.

"Juzi tulisikia huko Kilimanjaro taasisi moja inafundisha walimu wetu wa shule haya mambo ambayo sisi hatukubaliani nayo kwa sababu yanakiuka mila, desturi na utamaduni zetu.

"Mkuu wa wilaya amewapiga stop (amewakataza) wamebeba walimu kwenda Zanzibar kwenda kuwafundishia huko. Wewe Katibu Tawala upo na watumishi wako, wanabebwa kupelekwa Zanzibar, lazima ujue mizunguko ya watumishi wako, nendeni mkasimamie ajenda za kitaifa," alisema.

Majaliwa pia alisema kuna migogoro mingi ya ardhi na makatibu hao kwenye maeneo yao na kuwataka wakaishughulikie ili waziri asilazimike kwenda kutatua.

Aliwataka kusimamia mwenendo wa vyama vya siasa, kujenga uhusiano wa kiutendaji, kuzingatia utumishi wa umma na kujiepusha na migongano ya maslahi.

Waziri Mkuu alisema kiongozi anatarajiwa kusikika kwa lugha ya matumaini, hamasa na uzalendo ili wengine wakuige.

"Huu ndiyo wakati unaotakiwa kuacha zile ulizokuwa unavaa huko, ukivaa watu waseme huyu DAS, lazima ubadilike kwa mavazi, mienendo ya tabia baada ya kuteuliwa lazima mwenendo wako ubadilike, tunajua kuna wengine ni mahiri katika kucheza muziki mpaka unakuwa bingwa, hatuhitaji uwe bingwa wa muziki.

"Tembea na flashi yenye muziki, weka kwenye gari tikisa mabega, hapo ndo mwisho wako, katika kumbi za starehe lazima ukwepe. Suala la ulaji - haiwezekani kwenye sherehe ionekane DAS umejaza chakula hadi kinadondoka.

"Mihemko ya aina yoyote lazima uweze kuidhibiti, wewe ni wa kujadili, kusikia na kutoa miongozo, DAS lazima uwe na mipango ya kazi," alisema.

Waziri Mkuu alisema viongozi hao wanategemewa katika kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM na maelekezo yanayotolewa na viongozi wa juu na mafunzo hayo yatawasaidia kuwapa uelewa mpana wa kutekeleza majukumu yao.

Aliwahimiza kusimamia tabia za watumishi wa umma na kutunza siri za serikali huku akiwaagiza kusimamia ipasavyo kila sarafu ya fedha iliyoingia katika halmashauri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema kuwa mwezi Desemba mwaka jana, ofisi yake ilitatua migogoro kadhaa baina ya makatibu hao, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

"Sitarajii kuona migogoro, nikiona nitawaita na kushauriana na mamlaka kwamba hamtoshi kuendelea katika nafasi hiyo. Kuna baadhi ya ofisi za wakuu wa wilaya hazina mipango kazi, lazima uenende na hadhi yako unavyoanza kuanika mambo yako ya familia kwenye mitandao sisi tunataka kuona kazi zaidi," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema mafunzo hayo yamehudhuriwa na makatibu hao 135 na yalenga kuimarisha usimamizi wa utendaji kazi wao.

# Wasafirishaji watoa fedha kutatua kero ya uhaba miundombinu shuleni

**Na Mwandishi Wetu**, GEITA

KAMPUNI ya kusafirisha bidhaa mbalimbali ya Blue Coast ya mjini Geita, imetoa Sh. milioni 52.7 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi Mseto na Nyamalembo.

Wasafirishaji hao wametoa fedha hizo kwa lengo la kutatua kero ya uhaba wa miundombinu na samani rafiki kwa ujifunzaji na ufundishaji shuleni.

Meneja wa Kampuni ya Blue Coast Geita, Jeremiah Musa, katika hafla ya kukabidhi vyumba vya madarasa kwa shule hizo juzi, alisema fedha hizo ni sehemu ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR).

Kwa mujibu wa meneja huyo, fedha hizo zimetumika kujenga madarasa mawili na kununua samani zake.

Alisema kampuni hiyo inaamini mafanikio yake yanaambatana na uwajibikaji kwa jamii kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za elimu, afya na michezo katika Mkoa wa Geita.

Mkurugenzi wa Blue Coast Tanzania, Athanas Inyas, alisema mazingira mazuri ya kufanya biashara yanayotengenezwa na serikali ni chachu kwa wafanyabiashara hasa wazawa kunufaika na uwekezaji.

Alisema kampuni hiyo itaendelea kutoa kwa jamii ili kuhakikisha inakuwa na mazingira mazuri ya kufanya kazi, huku akiahidi kupaka rangi madarasa yote ya Shule ya Msingi Nyamalembo ambayo ni chakavu na hayaonyeshi taswira nzuri kwa jamii.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyamalembo yenye wanafunzi zaidi ya 1,000, Josia Mombeki, alisema inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Alibainisha kuwa kwa sasa, wanafunzi 100 wanatumia chumba kimoja cha darasa, hali inayowapa ugumu kuelewa mwalimu anapofundisha.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, kwa ufundishaji na ujifunzaji wenye tija, chumba kimoja cha darasa kinapaswa kutumiwa na wanafunzi wasiozidi 45.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mseto, Nyimbona Matiti, alisema uchakavu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa katika shule unahatarisha usalama wa wanafunzi na walimu, pia unachangia utoro kwa wanafunzi.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella, akipokea madarasa hayo, alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Sh. bilioni 9.7 zimetolewa kupitia mradi wa Boost kwa ajili ya miradi ya elimu katika mkoa huo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina (kulia), akizungumza na mafundi wakati akikagua ujenzi wa madarasa mapya katika shule mbalimbali wilayani humo jana, yanajengwa kwa fedha za mradi wa Boost. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Majaji wamvaa Rostam Aziz

**Na Jenifer Gilla**

MFANYABIASHARA Rostam Aziz amekiomba radhi Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT) kutokana na kauli aliyoitoa dhidi ya mahakama.

Rostam ameomba radhi ikiwa ni saa chache baada ya JMAT kutoa taarifa kwa umma, kumtaka mfanyabiashara huyo athibitishe tuhuma alizotoa dhidi ya mahakama au aombe radhi hadharani.

Juni 26 mwaka huu, mfanyabiashara huyo akizungumza mbele ya waandishi wa habari, alitoa kauli ambayo ndiyo imesababisha chama hicho kumtaka aombe radhi.

Katika kauli yake siku hiyo alisema: "Hakuna mwekezaji atawekeza kwenye nchi ambayo kesi ikipelekwa hapo Kisutu kiongozi yeyote anaweza kupiga simu akaielekeza mahakama nini cha kufanya."

Kwa mujibu wa taarifa ya JMAT, mfanyabiashara huyo wakati akizungumza na waandishi wa habari, aliituhumu Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa kutokuwa huru katika uendeshaji wa shughuli zake, jambo wanalodai siyo kweli.

"Kutokana na taarifa hiyo tunapenda kubainisha yafuatayo: "Hakuna jaji aliyetoa huduma katika mahakama hiyo kama ilivyoripotiwa na mzungumzaji wa taarifa hiyo," ilieleza sehemu ya taarifa ya JMAT.

Kutokana na hilo, chama hicho kilisema kimesikitishwa na kauli ya Rostam ambaye hawakutegemea aongee mambo mazito kama hayo bila kuwa na uhakika wala uthibitisho.

"Matamshi ya Rostamu Aziz yanaweza kuhatarisha uhusiano na ushirikiano katika mihimili mitatu ya dola ndani ya nchi yetu.

"Tunaomba wananchi wenye nia njema na mahakama na mihimili mingine waendelee kuwa na imani na mfumo wa utoaji haki nchini.

"Kwa taarifa hii Chama cha Majaji na Mahakimu Tanzania kinamtaka Rostam Aziz athibitishe kauli yake akibainisha jina la jaji na lini alipewa maagizo na kiongozi wa serikali kutoa uamuzi kinyume cha taratibu. Akishindwa kutoa uthibitisho, tunamtaka atumie jukwaa lile lile kuomba radhi kwa uzito uleule," ilisema taarifa hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari nyumbani kwake, Rostam alisema halikuwa lengo lake kudharau mahakama, bali ulimi uliteleza.

"Nimesoma taarifa ya Chama cha Majaji na Mahakimu, na kwa sababu ya kutambua na kuheshimu dhima, hadhi na wajibu wa kikatiba na mahakama, ningependa kuuhakikishia umma kwamba wakati ninazungumzia uwekezaji, halikuwa kusudio langu kudharau mahakama zetu," alisema Rostam.

Alisema kusudio lake lilikuwa ni kulenga uwekezaji nchini na kuwavutia wawekezaji kwamba "...haina budi kufuata sheria na taratibu za kimataifa ambazo zinataka kunapokuwa na migogoro ya kimataifa katika uwekezaji ikashughulikiwe katika mahakama za kimataifa."

Alisema wawekezaji wanahitaji mahali pa kwenda kunapotokea migogoro na sheria ya kimataifa ipo wazi kuwa wahusika watakwenda kusuluhishwa na majaji ambao hawahusiki na upande wowote.

"Kusudio langu lilikuwa ni kuelimisha wale wanaosema kwamba kwa nini tukiwa na mgogoro tunakwenda nchi nyingine kusuluhishwa. Huu ndiyo utaratibu wa dunia nzima, siyo Tanzania," alifafanua Rostam.

HABARI MICHEZO

# DODOMA JIJI YAFUMUA KIKOSI, KUBAKI NA WACHEZAJI 27 TU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imesema itafanya marekebisho makubwa kwenye kikosi cha msimu ujao kwa kusajili wachezaji karibuni maeneo yote, huku ikipunguza idadi ambayo haitozidi 27.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili wa klabu hiyo, Fredrick Mwakisambwe, amesema kutoka jijini Dodoma kuwa ripoti ya benchi la ufundi imeonyesha kuwa kikosi chao kinatakiwa kufanyiwa marekebisho makubwa kwa kusajili wachezaji kila idara ili kiwe na uwezo wa kupambana na kuhimili mikikimikiki ya Ligi Kuu msimu ujao.

“Tunafanya maboresho ya kikosi chetu karibuni maeneo yote kuanzia golikipa, upande wa beki, viungo na ushambuliaji, baada ya siku nne au tano, tutaanza kuwatajia maeneo ambayo tayari tumeyafanyia kazi kwa kuwatajia majina yao, mpaka sasa kuna wachezaji ambao tupo kwenye mazungumzo nao na yanakwenda vizuri tu,” alisema Mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, alisema msimu ujao watapunguza idadi ya wachezaji kwa ajili ya kuongeza ufanisi zaidi kwenye kikosi hicho.

“Hatutokuwa na wachezaji wanaozidi 27, ni idadi inayotosheleza kabisa kuwa na jeshi ambalo litafanya kazi kwa weledi, ufanisi na mafanikio,” alisema.

Alisema maboresho ya wachezaji wa Dodoma Jiji yanakwenda sambamba na marekebisho ya Uwanja wa Jamhuri Dodoma ambapo wanawashukuru wamiliki wa uwanja huo kwa kupunguza baadhi ya matumizi ambayo yalikuwa yakiufanya kutokuwa kwenye hali nzuri.

“Sisi tulichimba kisima ambacho kwa kiasi kikubwa kilichangia kuufanya uwanja kuwa kwenye hali nzuri, lakini tunawashukuru sana wamiliki wa uwanja kwa sababu hivi sasa wamepunguza sana matumizi yasiyo ya lazima ya uwanja ambayo mara nyingi yalisababisha uwanja kutokuwa na hali nzuri, nawahakikishia, msimu ujao uwanja utakuwa bora zaidi ya viwanja vingi nchini,” alisema Mwakisambwe.




Kikundi cha ngoma za asili cha Nyota kikitoa burudani kwenye hafla ya uzinduzi wa mradi wa ‘Hakuna Marefu Yasiyo na Mwisho’ jijini Dodoma juzi. Mradi huo unalenga kuwezesha watoto wa kike kutimiza ndoto zao kwa kuepuka ndoa za utotoni. **MPIGAPICHA WETU**

## Mfaume aomba radhi mashabiki

**Na Abdallah Mataka**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Mfaume Mfaume ‘Mapafu ya Mbwa’, amewaomba radhi mashabiki wake kutokana na kushindwa kuonesha kiwango kikubwa katika pambano lake dhidi ya Chikondi Makawa wa Malawi.

Mfaume alisema kuwa anaenda kuyafanyi kazi mapungufu yote yalijitokeza katika pambano hilo kuelekea pambano lake lingine dhidi ya Idd Pialali litakalofanyika Septemba mwaka huu.

Mwishoni mwa juma lililopita, Mfaume alifanikiwa kuibuka na ushindi wa pointi dhidi ya Chikondi Makawa katika pambano la utangulizi hiyo ikiwa ni mara ya pili kwa mabondia hao kukutana.

Licha ya ushindi huo, mashabiki na wapenzi wa masumbwi nchini havutiwa na kiwango alichokionesha Mfaume kwenye pambano hilo.

“Nashukuru Mungu kwamba nimeweza kupata matokeo katika pambano lile na Chikondi kwa sababu sikuwa nimejiandaa kwa ajili yake, lakini kutokana na mpinzani wangu kupata changamoto ikanibidi nicheze naye.

“Lakini nataka niwaambie mashabiki wangu, wanisamehe ila ahadi yangu kwao ni kuwa bora katika pambano langu lijalo mwezi wa tisa, naamini nitawapa furaha kubwa kwa mchezo mzuri,” alisema Mfaume.

Katika pambano hilo ambalo liliandaliwa na PAF Promotion Company Limited, Mfaume ilikuwa acheze na Nkululeko Mhlongo wa Afrika kusini anayeishi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kabla ya kubadilishiwa bondia na kupanda uliongoni dhidi ya Makawa kutoka Malawi baada ya Muhlongo kupata changamoto na kushindwa kufika katika pambano hilo.

# Mtibwa Sugar yapata mrithi wa Mayanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar umesema uko katika mchakato wa kufanya maboresho ya kikosi chao na benchi la ufundi kwa kumtangaza kocha mkuu atakayechukuwa nafasi ya Salum Mayanga.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Sabri Aboubakar, alisema katika kuhakikisha wanafanya vizuri msimu ujao, wanalazimika kufanya maboresho ya kikosi chao kuanzia benchi la ufundi.

Alisema tayari wameshampata mwalimu atakayekinoa kikosi cha timu hiyo ambaye amekidhi vigezo walivyovitaka, hivyo ni matarajio yao atafikia malengo kwa msimu ujao wa mashindano iliyopombele yao.

“Tumeweka vigezo vyetu na tayari tumempata kocha na muda wowote tutamtangaza mrithi wa Mayanga baada ya kumaliza baadhi ya taratibu za makubaliano na mwalimu huyo.

Pia kuna maboresho ya kikosi baada ya kufanya tathmini ya msimu wa 2022/23 kwa kupitia ripoti ya benchi la ufundi tunatakiwa kusajili nyota sita katika nafasi tatu muhimu,” alisema Sabri.

Aliongeza kuwa wanapaswa kuwa makini zaidi katika safu ya ulinzi ambayo msimu uliopita haikuwa bora na kuchangia kutokufanya.

“Mchakato wa usajili umefanyika kwa umakini katika nafasi ya ulinzi ilikuwa tatizo kubwa, pia tutasajili viungo wawili na washambuliaji wawili,” alisema Ofisa Mtendaji huyo wa Mtibwa Sugar.

Kuhusu kupandisha baadhi ya wachezaji kutoka timu yao ya vijana ya U-20 na mshambuliaji Athuman Masumbuko (Makambo), alisema ni miongoni mwa nyota waliopendekezwa kupandishwa timu kubwa.

Sabri alisema wanasubiri taarifa kutoka benchi la ufundi na wanatarajia kuchukuwa wachezaji kutoka kikosi cha timu ya U-20 ambao ni mabingwa wa Ligi ya Vijana nchini.

Mtibwa Sugar ambayo msimu uliomalizika ilimaliza katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 35, safu yake ya ulinzi iliruhusu mabao 45 huku ile ya ushambuliaji ikiwezesha kupatikana mabao 34.

## ZISIKUPITE

### BAYERN OFA YA PILI
BAYERN Munich inapanga kuwasilisha ofa ya pili kwa Klabu ya Tottenham Hotspur kwa lengo la kumnunua mshambuliaji wao, Harry Kane, 29. **(Sky Sporti)**

### CITY YAKOMAA NA GVARDIOL
KLABU ya Manchester City inatayarisha ofa yao ya kwanza ya kumnunua mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuanza mazungumzo na RB Leipzig. **(ESPN)**

### NYOTA WATAKIWA SAUDIA
KIUNGO wa Liverpool na England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 33, na mshambuliaji wa Chelsea na Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 34, ni wachezaji wawili wanaoweza kusajiliwa na Al-Ettifaq baada ya klabu hiyo ya Saudi Arabia kumteua Steven Gerrard kama kocha wao mpya. **(Mail)**

### VEIGA AWINDWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain inapania kuzishinda Chelsea, Liverpool na Manchester City katika mbio za usajili wa kiungo wa Hispania, Gabri Veiga mwenye umri wa miaka 21, kutoka Celta Vigo. **(Guardian)**

### TINO AWANIWA CHELSEA
CHELSEA imefanya mazungumzo na Southampton kuhusu uwezekano wa kumnunua beki wao, Tino Livramento mwenye umri wa miaka 20. Southampton wamepanga bei ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 21, ambaye anawindwa na Newcastle, kwa pauni milioni 38. **(Mail)**

### LAVIA KWA CHELSEA, LIVER
LIVERPOOL imepiga hatua mbele ya Chelsea katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia na wanaandaa ofa ya ufunguzi kwa kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye Southampton wanasema thamani yake ni pauni milioni 50. **(talkSPORT)**

### ONANA APEWA OFA SAUDIA
KLABU ya Al-Nassr imetoa ofa nono kwa golikipa wa Cameroon na Inter Milan, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27, ambaye analengwa na Manchester United. **(CBS)**

### XHAKA ANUKIA LEVERKUSEN
KIUNGO wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 30, atakamilisha uhamisho wa pauni milioni 21.5 kwenda Bayer Leverkusen wiki hii. **(Sun)**

### TOURE ATAKIWA EVERTON
KLABU ya Everton imeiambia Almeria kwamba wanania ya kufikia kipengele cha kuachiwa kwa El Bilal Toure cha euro milioni 40, ingawa Fulham wanaweza kumnunua mshambulizi huyo wa Mali mwenye umri wa miaka 21, ikiwa watamuuza mshambuliaji wa Serbia, Aleksandar Mitrovic mwenye umri wa miaka 28 msimu huu wa majira ya joto. **(Sacha Tavolieri)**

### NEWCASTLE YAMTAKA INACIO
KLABU ya Newcastle United inatafakari uwezekano wa kumnunua beki wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio, 21. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PULISIC AKATAA KWENDA LYON, AITAKA AC MILAN

●●● Ataka kucheza klabu inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwamba...

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Christian Pulisic, amekataa kujiunga na Lyon msimu huu wa majira ya joto, akipendelea kuhamia AC Milan baada ya kukubaliana kimsingi na klabu hiyo ya Ligi Kuu Italia, Serie A, vyanzo vimeiambia ESPN.

Lyon wamewasilisha ofa kwa Chelsea kwa nyota huyo wa Marekani, ingawa ni chini ya ada inayotakiwa ya euro milioni 25.

Lyon pia haiwezi kufikia ofa ya mshahara iliyotoa Milan.

ESPN iliripoti Ijumaa kwamba Pulisic alikuwa amekubaliana maslahi binafsi na Milan, na vyanzo viliiambia ESPN klabu hiyo ya Italia inakusudia kutoa ofa iliyoboreshwa baada ya kuona ombi lao la awali la euro milioni 15 limekataliwa na Chelsea ambao wanataka euro milioni 25 ili kumuachia Pulisic.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Pulisic haoni Lyon kama hatua sahihi kwake, badala yake anataka kucheza katika klabu inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo ipo huko.

Pulisic alifurahia kipindi kizuri cha mapema akiwa Chelsea baada ya kujiunga kwa mkataba wa euro milioni 64 mwaka 2018 kutoka Borussia Dortmund, lakini tangu wakati huo amekuwa akisumbuliwa na majeraha.

Muda wake wa kucheza Chelsea pia umezidi kuwa mdogo huku kukiwa na washambuliaji kadhaa, wakiwamo Mykhailo Mudryk, Raheem Sterling, Noni Madueke, David Datro Fofana, Christopher Nkunku na Nicolas Jackson.

Pulisic amecheza mechi 145 katika misimu minne akiwa na Chelsea, wakati ambapo alikuwa sehemu ya klabu hiyo iliyoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021.

Pia aliisaidia kunyanyua taji la UEFA Super na Kombe la Klabu Bingwa Dunia mwaka huo.



# GERRARD NAYE ATUA SAUDIA

**DAMMAM, Saudi Arabia**

STEVEN Gerrard limekuwa jina jingine kubwa la hivi karibuni zaidi kuhamia kwenye soka la Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Saudi Pro League, baada ya kuteuliwa kuwa meneja mpya wa Al Ettifaq.

ESPN iliripoti kwamba kocha huyo mwenye umri wa miaka 43, alianza tena mazungumzo na klabu hiyo baada ya awali kukataa ofa ya kujiunga nao mwezi uliopita.

Nahodha huyo wa zamani wa Liverpool, ambaye alitimuliwa na Aston Villa Novemba mwaka jana ikiwa ni chini ya miezi 12 akiwa pale Villa Park, sasa atachukua jukumu la kuinoa klabu hiyo yenye maskani yake Dammam.

Kwa mujibu wa ESPN, Gerrard alikuwa tayari kuhamia Saudi Arabia baada ya majadiliano zaidi na uongozi wa klabu.

"Mahali ambapo magwiji wanapatikana. Tunafuraha kumtangaza Steven Gerrard ndiye kocha wetu mpya," ilisomeka taarifa ya Al-Ettifaq ikiandikwa kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Yeye si mgeni. Ni gwiji ambaye analeta historia tukufu na mustakabali wa kusisimua kwa Ettifaq," iliongeza taarifa hiyo.

Rais wa Klabu, Khalid Al-Dabal, alionesha furaha yake baada ya Gerrard kusaini mkataba wa miaka miwili.

Al-Dabal alielezea mpango huo kama moja ya maarufu na ushawishi mkubwa katika Ligi ya Saudi Pro League.

Al Ettifaq ilikuwa haina kocha wa kudumu tangu kocha Mfaransa Patrice Carteron alipoondoka katika klabu hiyo Februari mwaka huu.

Lakini wamemteua Gerrard kama chaguo lao la kuijenga upya timu hiyo baada ya kumaliza nafasi ya saba kwenye Ligi Kuu yenye timu 16 msimu uliopita - pointi 35 nyuma ya mabingwa Al Ittihad, ambao wamemuongeza fowadi wa Real Madrid, Karim Benzema kwenye kikosi chao.

Gerrard, ambaye aliiongoza Rangers kutwaa taji lao la kwanza la Scotland ndani ya miaka 10 mwaka 2021, alikuwa pia anahusishwa na nafasi za ukocha katika Klabu za Leicester City na Leeds United - zote zilishuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliopita.

Nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya England anajiunga na kundi la watu mashuhuri waliotimkia Saudi Arabia hivi karibuni, wakiwamo Benzema, Cristiano Ronaldo na N'Golo Kante.

# Pochettino: Tunataka kuleta furaha Chelsea

**LONDON, England**

MAURICIO Pochettino anatazamia kupanga mipango ya kuijenga upya Chelsea na kurejesha furaha.

'The Blues' hao walimaliza katika nafasi ya 12 kwenye Ligi Kuu England wakiwa na pointi 44 msimu uliopita, wakijikusanyia ushindi mara 11 pekee katika mechi 38.

Lakini sasa kuna matumaini makubwa pale Stamford Bridge baada ya kuwasili kwa Pochettino, pamoja na kusajiliwa kwa washambuliaji Christopher Nkunku na Nicolas Jackson.

Pochettino mwenye umri wa miaka 51, alisema: "Tunataka kuleta furaha tena kwa klabu hii kubwa ya soka.

"Historia ya Chelsea ni kushinda, lakini ni muhimu jinsi tunavyoenda kujenga ushindi huo.

"Katika miaka 10, 12, 15 iliyopita, Chelsea ndiyo timu kubwa zaidi nchini England. Nataka kuifanya iwe ya kusisimua sana kufanya kazi na timu yetu changa na tunaweza kujenga mafanikio katika miaka michache ijayo."




Pochettino anafurahia fursa hiyo ya kuboresha wachezaji wachanga wenye vipaji wa klabu hiyo.

Aliongeza: "Matarajio ni sisi kwanza kuunda jukwaa kwao kujisikia vizuri sana kwenye uwanja wa mazoezi.

"Wanahitaji kuwa na nafasi yao na kujisikia muhimu.

"Utaalamu wetu ni kuipa Chelsea zana bora zaidi kwa wachezaji kuwa na mafanikio, kuboresha kwa njia ya mtu binafsi na ya pamoja, na nadhani tuna uzoefu na kwa pamoja tunaweza kuunda safari nzuri.

"Ikiwa sote tutakuwa pamoja tutakuwa na nguvu kwa sababu tuna kikosi bora na tutaleta wachezaji wenye kujitolea ambao wanataka kuwa sehemu yake."

# Bellingham atoboa siri ya Beckham Madrid

**MADRID, Hispania**

JUDE Bellingham amefichua kuwa David Beckham alimtumia ujumbe wa bahati nzuri baada ya kujiunga na Real Madrid.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 20, amekuwa mchezaji wa saba wa England kujiunga na klabu hiyo ya Bernabeu baada ya uhamisho wake wa euro milioni 103 kutoka Borussia Dortmund mwezi uliopita, akifuata nyayo za Beckham, Gareth Bale na Michael Owen.

Beckham labda ndiye aliyekuwa hadhi ya juu zaidi kuhamia mji huo mkuu wa Hispania mwaka 2003 kutoka Manchester United, ambao ulizidisha hadhi yake ya kimataifa, na nahodha huyo wa zamani wa England aliwasiliana na Bellingham kumtakia heri.

Na nyota huyo mpya wa Bernabeu alisema huenda akapata ujuzi wa Beckham na wachezaji wengine wa zamani wa kucheza Madrid.

"David Beckham alinitumia ujumbe mfupi wa kunitakia kila la heri," alisema Bellingham akiliambia Shirika la Habari la PA.

"Ni moja ya hatua ambazo kila mtu ana maoni yake kutoka nje kwa hiyo unasikia mambo mengi na ushauri, mimi ni mzuri katika kuchuja mazuri kutoka ubaya, hadi sasa imekuwa chanya kutoka kwa wachezaji wa zamani.

"Nitajaribu kuchukua hiyo kwenye bodi na wakati fulani labda nitawasiliana nao na kuona jinsi walivyozoea maisha ya Hispania."

Moja ya mambo ambayo Bellingham atakuwa akifanya ili kuzoea mtindo wake mpya wa maisha nchini Hispania na kujifunza lugha hiyo.

Kiungo huyo ameanza kutumia programu ya kujifunzia, akilenga kuendeleza misamiati mingi ili apate nafasi ya kwasiliana bila tabu.

"Nimeiweka yote kwenye simu yangu, nina mfululizo mzuri unaoendelea dakika hii," aliongeza. "Ni siku tisa tangu nianze kuichukulia lugha hii kwa uzito.

"Ni moja ya mambo ambayo unaisikia na unaanza kuchukua vitu vidogo na unaiona kwenye TV na mahojiano ya wachezaji wengine, kwa hiyo inakuja kawaida zaidi kuliko unavyofikiria.

"Ni rahisi zaidi kuliko kujaribu kujifunza Kijerumani. Nilisoka Kihispania shuleni hadi mwaka wa tisa, ni wazi, kwa kuzingatia nyuma, ningeendelea nayo.

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAALIKWA KUKIPIGA BURUNDI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Namungo FC imepata mwaliko kutoka Shirikisho la Soka la Burundi (FFB), kwa ajili ya kwenda kucheza mchezo maalum wa kirafiki wa kimataifa mwishoni mwa mwezi huu, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka mkoani Lindi, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Mkadeba, alisema wamepata mwaliko huo, lakini hawajajua wanakwenda kucheza na timu gani.

"Shirikisho la Soka Burundi limesema tuvute subira, litatufahamisha timu ambayo tutacheza nayo, kwetu tumeupokea mwaliko huo kwa mikono miwili," alisema Mkadeba.

Aidha, katibu huyo alisema Julai 10, wanatarajia kuelekea wilayani Karatu kuweka kambi ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza Agosti mwaka huu.

Alisema wamechagua kuweka kambi mkoani humo kutokana na kuwa na miundombinu mizuri ya viwanja vya mazoezi pamoja na gym za kisasa.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Denis Kitambi, alisema baada ya kumaliza kusaini mkataba wa miaka miwili na aliyekuwa mchezaji wa timu ya Simba, Erasto Nyoni, kwa sasa anaendelea kuwachunguza nyota wengine watatu anaowahitaji.

"Baada ya kumalizana na Erasto Nyoni nipo kwenye mazungumzo ya mwisho na wachezaji ambao ninawahitaji kwa lengo la kuiongezea nguvu timu yangu," alisema Kitambi.

Namungo imemaliza msimu uliopita ikiwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kujikusanyia pointi 40.



Wanariadha wakianza kukimbia katika mbio za Lake Victoria Marathon zilizofanyika jijini Mwanza mwishoni mwa wiki na kukutanisha mamia ya washiriki kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi. Mbio hizo zilidhaminiwa na Benki ya KCB Tanzania. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashindano ya gofu kufanyika Gymkhana

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO makubwa ya mchezo wa gofu yamepangwa kufanyika siku ya kilele cha maonyesho ya biashara (Sabasaba) Julai 7, mwaka huu kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Mashindano hayo yaliyodhaminiwa na Kampuni ya 'Lake Energy Group' yatahusisha watoto na watu wazima.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Mauzo wa kampuni hiyo, Stephen Munguti, alisema watatoa zawadi kwa washindi wa mashindano hayo ambayo lengo lake ni kuisapoti serikali katika juhudi zake za kuibua vipaji na kuendeleza michezo nchini.

Munguti alisema wanafahamu kuwa michezo ni ajira inayolipa kama zilivyo nyingine, hivyo wanaamini kupitia mashindano hayo, wataibua vipaji vitakavyotamba baadaye katika klabu mbalimbali na hatimaye kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kimataifa.

"Lake Energy Group tumeona ni vema tukaungana na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika jitihada zake za kupromoti michezo na wanamichezo.

"Tunafahamu pamoja na masomo, watoto wanatakiwa pia kujengwa kimwili na kiafya kiujumla, hivyo kupitia mashindano haya watakuwa wameimarika kiafya na kujenga tabia ya kushiriki katika michezo mara kwa mara kama itakavyokuwa kwa washiriki wengine," alisema Munguti.

Kwa upande wa Mratibu wa Mashindano hayo, Fredrick Laiser, alisema wamefanya hivyo ili kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto na watu wazima katika mchezo huo maarufu duniani.

Aidha, aliwashukuru Lake Energy Group kwa kukubali kudhamini mashindano hayo huku akiwataka wadau zaidi kujitokeza kuwasapoti ili kuzidi kuyanogesha mashindano hayo katika siku za usoni.

"Tunawaalika wazazi na walezi wa watoto watakaoshiriki na wadau wa mchezo wa gofu na wanamichezo kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi pale Gymkhana Club kushuhudia vipaji katika mchezo wa gofu," alisema Laiser.

## Yanga yabeba medali, makombe

INATOKA UK. 24

kuwa kumbukumbu kwenye historia ya klabu hiyo.

"Hakuna kitu cha kipekee kama mnafika ugenini, halafu mnawaonyesha mafanikio yenu, tunataka waone mafanikio yetu tuliyoyapata msimu huu, waone medali za fainali kwani sisi ndiyo timu pekee (msimu ulioisha) kwa ukanda huu wa Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na medali ya michuano inayosimamiwa na CAF, kwa hiyo mafanikio ya Yanga kuanzia wachezaji, viongozi, yataambatana na mataji kuelekea nchini Malawi, hii haina mjadala," alisisitiza.

Yanga imepata medali hizo, baada ta kufika hatua ya fainali ya Shirikisho la Soka barani Afrika kwa kucheza dhidi ya USMA ya Algeria iliyotwaa ubingwa.

Yanga ilikosa ubingwa kwa bao la ugenini, licha ya kushinda bao 1-0 ugenini, lakini nayo iliruhusu kufungwa mabao 2-1 nyumbani.

Mbali na medeli hizo, Yanga ilitwaa Ngao ya Jamii mapema mwanzoni mwa msimu ulioisha, kabla ya kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara 2022/23 na Kombe la FA.

## Robetinho anogesha

INATOKA UK. 24

sababu ni kwamba tunataka kupata utulivu, kupata huduma zote , eneo tulivu, viwanja bora vya kufanyia mazoezi, tunataka kupata mechi nyingi nzuri za kirafiki dhidi ya timu bora zenye viwango vikubwa, ukijumlisha yote hayo, tumeona huko kunatufaa kufanya maandalizi mazuri ya 'pre season', hivyo rasmi tunatoa taarifa kwa Mnyama Simba anakwenda zake Uturuki kwenda kujifua," alisema.

Aliitaja sababu ya ziada kuwa huko ndiko kulikochezwa fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliomalizika kati ya Manchester City ya England dhidi ya Inter Milan ya Italia Juni 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Atatürk Olympic jijini Istanbul, Man City ikishinda bao 1-0 na kutwaa ubingwa.

Ahmed alisema kwenda Uturuki pia ni mapendekezo ya Robertinho kupata muda wa wiki tatu hadi nne kwa ajili ya kukaa na wachezaji wake katika mazingira mazuri yenye utulivu ili kuandaa timu iliyo imara.

"Nadhani mmeona taarifa yetu kwamba tunaelekea nchini Uturuki kwa ajili ya kuweka kambi kuelekea msimu unaokuja, kila kitu kimewekwa vizuri na kocha Robertinho amewashawasili nchini akiwa na baadhi ya wasaidizi wake.

Kikosi kitaondoka nchini Julai 11, mwaka huu baada ya wachezaji wote kufika, waliokuwapo tangu awali na wapya watakuwa wamewasili kabla ya Julai 11, mwaka huu na kuwapo katika msafara huo," alisema Ahmed.

Akizungumzia usajili, Ahmed alisema bado wao wanaendelea na usajili ingawa tayari wameshasajili baadhi ya wachezaji.

"Wachezaji tuliowasajili na tunaendelea kuwasajili wataonekana siku hiyo uwanja wa ndege siku ya safari, maana mipango yao yote itakuwa imeshakamilika, hiyo ina maana wiki hii tutawatangaza wachezaji wetu wote tuliowasajili na kwenye suala hili niwathibitishe mashabiki wa Simba kuwa mambo ni mazuri, tumedhamiria kufanya usajili babkubwa na sisi wachezaji wetu siyo wale waliopewa 'thank you' na klabu zingine.

"Sisi tunasajili wachezaji ambao tunanyang'anyana sokoni, yaani klabu yake inamtaka, zingine hadi za Afrika na Ulaya zinawataka, kwa hiyo aina hiyo ya usajili huwa inachukua muda kidogo, kama ingekuwa ni wale walioachwa au hawana timu, saa hizi tungekuwa tumeshamaliza siku nyingi.

Mmoja wa wachezaji ambao Simba inatarajiwa kumtangaza ni beki wa kati Che Fondoh Malone ambaye pia inadaiwa alikuwa akiwaniwa na FC Zurich ya Uswisi.

Simba inatarajia kuondoka nchini Julai 11, mwaka huu kuelekea Uturuki kabla ya kurejea baada ya wiki tatu kwa ajili ya Tamasha lao la Simba Day na baadaye kuanza mikikimikiki ya Ligi Kuu Tanzania Bara na CAF Super League.

Licha ya kutowaweka wazi wanawasili lini gazeti hili limepata taarifa kuwa tayari nyota hao wameanza kuwasili tangu usiku wa juzi.

Baadhi ya nyota wanaotajwa ni Willy Onana kutoka Klabu ya Rayon Sport ya Rwanda, Beki Mcameroon Che Fondoh Malone na Efoe Novon kutoka Klabu ya Asko Kara ya Togo.

**Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo**

# Michezo

Jumatano Julai 5, 2023

Nipashe



**Pulisic akataa kwenda Lyon, aitaka AC Milan** UKURASA 21

# ROBETINHO ANOGESHA USAJILI SIMBA SC

## ●●●Atua na Mbrazili mdaka 'risasi', mastaa wapya wawasili, yatoa sababu kwenda Uturuki...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, akiwasili nchini alifajiri ya jana pamoja na kipa mpya, Mbrazili Caique Luiz Santos da Purificacao, klabu hiyo imesema inaendelea kufanya usajili huku ikitoa sababu muhimu za kwenda kuweka kambi ya wiki tatu nchini Uturuki kujiandaa na msimu ujao.

Kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, kilieleza kuwa Robertinho ametua na kipa huyo ambaye ni mbadala wa Beno Kakolanya aliyemaliza mkataba na timu hiyo, lakini akitarajiwa kuanza kulinda lango la Simba kutokana na Aishi Manula kuwa nje kwa kipindi cha miezi minne akiuguza jeraha baada ya kufanyiwa upasuaji mwezi uliopita.

Kuhusu kwenda kuweka kambi Uturuki, akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wameamua kwenda mji mkuu wa nchi hiyo, Ankara kwa ajili ya kuwapa utulivu wachezaji wao, kupata viwanja bora vya kufanyia mazoezi pamoja na vifaa vya kisasa, lakini kupata mechi kadhaa za kirafiki na timu nzuri, bora na zenye viwango vikubwa.

Ahmed alisema kikosi cha wachezaji wa Simba kitaondoka mapema wiki ijayo kikiwa na wachezaji wake wote mpaka wale wapya ambao wamesajiliwa msimu huu.

"Baada ya majadiliano ya viongozi na benchi la ufundi, hatimaye tumefikia mwafaka kwenda Uturuki kwenye jiji la Ankara ambako ndiko tunaenda kuweka kambi yetu na

UKURASA. 23




Caique Luiz Santos da Purificacao

## Yanga yabeba medali, makombe safari ya Malawi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema mbali na wachezaji pamoja na viongozi wataondoka leo kwenda nchini Malawi kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe za uhuru wa nchi hiyo, pia watakusanya mataji yote waliyoyapata msimu huu pamoja na medali za fedha zilizopatikana baada ya kufanikiwa kufika fainali ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na kwenda nayo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema jana jijini Dar es Salaam, haitokuwa na maana kuondoka na wachezaji wakiyaacha mataji yao ambayo yamewafanya kupata heshima kubwa Afrika kwa sasa.

Yanga ambayo imepata mwaliko maalum kutoka Serikali ya Malawi chini ya Rais wa nchi hiyo Lazarus Chakwera kuhudhuria maadhimisho ya miaka 59 ya uhuru yatakayofanyika kesho, inatarajiwa pia kucheza na Nyasa Big Bullets, Uwanja wa Bingu Mutharika, uliopo Lilongwe nchini humo.

"Kuhusu makombe, mataji na medali, vyote vitaambatana na wachezaji na viongozi wa Yanga mpaka Malawi, na kila mchezaji wakati wa kuondoka itabidi avae medali yake ya CAF tulizozipata baada ya kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, na huyu mchezaji mpya ambaye tutaondoka naye nitampa ya kwangu avae," alisema Kamwe.

Alisema isingewezekana kwenda huko bila kuwaonyesha mafanikio ambayo wameyapata kwa msimu huu bora na utakaobaki

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >